**TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA**

# MTAALA WA SHULE YA JUNIA

# KISWAHILI

## GREDI YA SABA

Toleo la Kwanza 2022

Iliyorekebishwa 2024

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa mtaala huu kwa njia yoyote ile bila idhini, kwa maandishi, ya mchapishaji.

**ISBN: 978-9914-43-937-3**

Kimechapishwa na Kutolewa na Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya

## DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU

Serikali ya Kenya imejitolea kuhakikisha kuwa malengo ya sera kuhusu elimu, mafunzo na utafiti yanatimiza malengo ya Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya Kenya 2030, Sera ya Mtaala ya Kitaifa 2019, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa na Mikataba ya Kikanda na ya Kimataifa ambayo Kenya ni mshirika. Katika kutimiza lengo la Elimu ya Msingi, Wizara ya Elimu imefanikiwa kutekeleza hatua kwa hatua Mtaala wa Kiumilisi katika viwango vya Chekechea, Shule ya Msingi na katika Daraja ya Awali ya shule za upili.

Utekelezwaji wa Mtaala wa kiumilisi, unahusisha, kuangalia mara kwa mara vile unaendelea kutekelezwa ili kutathmini utekelezwaji wake. Miaka mitano baada ya kutekelezwa kwake, tathmini tamati ya utekelezwaji ulifanywa katika shule za msingi ili kubainisha ufanisi wake kama inavyopendekezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF). Serikali ya Kenya iliunda Tume ya Rais ya Elimu ya kushughulikia masuala mbalimbali, yanayoathiri sekta ya elimu nchini mwaka wa 2022. Tume hii ilitoa mapendekezo mbalimbali, yaliyochangia marekebisho ya mtaala. Mapendekezo ya tume hii, ripoti za tathmini, tathmini tamati zilizofanywa, mapendekezo kutoka kwa washikadau, na wale wanaotekeleza mtaala yalisababisha hatua ya kufanya marekebisho katika mtaala pamoja na kuchunguza upya masomo yaliyopendekezwa.

Mitaala ya Gredi ya 7 inaendeleza umilisi walioupata wanafunzi kufikia mwisho wa Gredi ya 6. Aidha, inatoa fursa kwa wanafunzi kuendelea kutalii na kukuza uwezo wao wanapojiandaa kujiunga na Daraja ya Juu ya Shule za Upili.

Mtaala huu unaeleza Malengo ya Elimu ya Kitaifa, kauli kiini, matokeo ya kijumla na maalum yanayotarajiwa kwa kila somo pamoja na mada na mada ndogo. Mtaala huu pia unabainisha Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa, Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa, umilisi wa kimsingi unaokuzwa, masuala mtambuko, maadili, shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji na vigezo na viwango vya kuzingatia katika kutathmini.

Ni matumaini yangu kuwa, mashirika yote ya serikali na wadau wengine wa elimu watatumia mtaala kuandaa utekelezaji fanifu na wenye tija wa Mtaala wa Kiumilisi.

**PROF. GEORGE A. O. MAGOHA, MBS, EBS, CBS**
**WAZIRI WA ELIMU**
**WIZARA YA ELIMU**

## DIBAJI YA KATIBU MKUU

Wizara ya Elimu imetekeleza Mtaala wa Kiumilisi ulioanza mwaka wa 2019. Gredi ya 7 ndiyo kiwango cha kwanza cha Daraja ya Awali Shule za Upili katika mpangilio mpya wa elimu.

Mtaala wa Gredi ya 7 uliofanyiwa marekebisho, unaendeleza utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi kutoka Gredi ya 6 katika shule za msingi. Sifa kuu ya daraja hii ni mtaala mpana unaomwezesha mwanafunzi kutalii talanta, hamu na uwezo wake kabla ya kuchagua mkondo wa masomo katika Daraja ya Juu Shule za Upili. Hili ni muhimu sana katika kutimiza ruwaza na lengo la mabadiliko ya mtaala yanayoendelea kama ilivyoelezwa katika Mswada Elekezi Nambari 1 wa mwaka 2019 wenye mada: *Kuelekea kufikia Elimu Bora, Faafu na Jumuishi na Mafunzo kwa Maendeleo Endelevu Nchini Kenya*. Mswada huu unafafanua mabadiliko kutoka kwa mtaala unaolenga kupokeza maarifa hadi mtaala unaolenga kukuza uwezo wa kila mwanafunzi.

Kwa hivyo, mtaala wa Gredi ya 7 unakusudiwa kuimarisha ukuaji wa mwanafunzi katika umilisi wa kimsingi wa Mtaala wa Kiumilisi ambao ni: mawasiliano na ushirikiano, uwazaji kina na utatuzi wa matatizo, ubunifu, uraia, ujuzi wa kidijitali, hamu ya ujifunzaji na kujiamini.

Mtaala huu unatoa Shughuli za ujifunzaji zilizopendekezwa husishi na tofautishi kuambatana na mada ndogo mbalimbali na vipengele vingine vya Mtaala wa Kiumilisi. Mtaala pia unapendekeza nyenzo za kufundishia pamoja na mbinu anuwai za kutathminia. Inatarajiwa kuwa mtaala huu utawaongoza walimu kikamilifu kuwaelekeza wanafunzi kufikia matokeo yanayotarajiwa katika Gredi ya 7 na kuwaandaa kuingia katika Gredi inayofuata bila tatizo. Vilevile, ni matumaini yangu kuwa walimu watautumia mtaala huu kuufanya ujifunzaji kuwa wa kuvutia, kuchangamsha na wenye kufurahisha.

**JULIUS O. JWAN, PhD, CBS**
**KATIBU MKUU**
**IDARA YA SERIKALI YA ELIMU YA AWALI NA ELIMU YA MSINGI**
**WIZARA YA ELIMU**

**SHUKRANI**

Sheria nambari 4 ya 2013 (iliyorekebishwa 2019) ya Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya inaipa mamlaka Taasisi kukuza mitaala na nyenzo za utekelezaji mtaala kwa elimu ya msingi na taasisi za elimu na mafunzo. Mchakato wa ukuzaji mtaala wa kiwango chochote cha elimu huhusisha utafiti wa kina, ulinganishi wa kimataifa na uhusishaji mkubwa wa wadau. Kupitia kwa mchakato uliopangwa kikamilifu na wa mashauriano, KICD ilibuni Mtaala wa Kiumilisi (CBC) kama ilivyoelezwa katika Utaratibu wa Mtaala wa Elimu ya Msingi (BECF) ambao unaitikia mahitaji ya karne ya 21 na matamanio yanayoelezwa katika Katiba ya Kenya ya 2010, Ruwaza ya 2030, Itifaki ya Jumuia ya Afrika Mashariki pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa.

KICD hupata ufadhili kutoka kwa Serikali ya Kenya ili kuwezesha ufikiaji kikamilifu wa majukumu na utekelezaji wa mipango ya Serikali na Sekta za Wizara ya Elimu. Taasisi pia inapata msaada kutoka kwa washirika wa maendeleo unaolenga miradi mahususi. Mtaala wa Gredi ya 7 umeandaliwa kwa ufadhili wa Benki ya Dunia kupitia mpango wa *Kenya Primary Education Equity in Learning Programme (KPEELP);* ulio chini ya uelekezi wa Wizara ya Elimu. Kwa hivyo, Taasisi inatoa shukrani za dhati kwa msaada kutoka kwa Serikali ya Kenya kupitia Wizara ya Elimu na washirika wengine wa maendeleo kwa sera na msaada wa mali na mikakati. Taasisi inatoa shukrani za kipekee kwa Waziri wa Elimu, Katibu Mkuu katika Idara ya Serikali ya Mafunzo ya Awali na Elimu ya Msingi.

Tungependa kuwashukuru wakuza mitaala wa KICD na wafanyakazi wengine, walimu wote na wakufunzi walioshiriki kama wanajopo katika ukuzaji wa mitaala. Nashukuru pia Mashirika Huru ya Serikali (SAGAs) na wawakilishi wa wadau mbalimbali kwa michango yao katika kuuandaa Mtaala wa Gredi ya Saba. Kwa mintarafu hii, tunatambua msaada wa Afisa Mkuu Mtendaji wa Tume ya Kuwaajiri Walimu (TSC) na Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza la Kitaifa la Mitihani nchini Kenya (KNEC) kwa usaidizi wao katika mchakato mzima wa kuuandaa mtaala. Mwisho, tunamshukuru Mwenyekiti wa Baraza la Taasisi ya Ukuzaji Mitaala Kenya (KICD) na wanachama wengine wa Baraza kwa uelekezi wao wa mara kwa mara katika mchakato huu.

Tunawahakikishia walimu wote, wazazi na wadau wengine kuwa mtaala huu utaelekeza ipasavyo utekelezaji wa Mtaala wa Kiumilisi katika Gredi ya 7 na uandaaji wa wanafunzi kuingia katika Gredi ya 8.

**PROF. CHARLES O. ONG'ONDO, PhD, MBS**
**MKURUGENZI/AFISA MTENDAJI MKUU**
**<u>TAASISI YA UKUZAJI MITAALA KENYA</u>**

## YALIYOMO

DIBAJI YA WAZIRI WA ELIMU ........ i
DIBAJI YA KATIBU MKUU ........ ii
SHUKRANI ........ iii
YALIYOMO ........ iv
MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA ........ vi
MGAO WA VIPINDI ........ viii
MATOKEO YA KIWANGO CHA KATI CHA ELIMU YA MSINGI ........ ix
KAULI KIINI ........ ix
MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA DARAJA LA AWALI LA SHULE ZA UPILI ........ x
MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO ........ xi
MWONGOZO WA KUTUMIA VITABU VYA KUSOMA SHULE YA JUNIA ........ xv
1.0 USAFI WA KIBINAFSI ........ 1
2.0 LISHE B0RA ........ 10
3.0 UHURU WA WANYAMA ........ 19
4.0 AINA ZA MALIASILI ........ 27
5.0 UNYANYASAJI WA KIJINSIA ........ 38
6.0 USALAMA SHULENI ........ 48
7.0 KUHUDUMIA JAMII SHULENI ........ 58
8.0 ULAGUZI WA BINADAMU ........ 67

9.0 MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA MAWASILIANO ........ 78
10.0 KIJITHAMINI ........ 88
11.0 MAJUKUMU YA WATOTO ........ 96
12.0 MAGONJWA AMBUKIZI ........ 106
13.0 UTATUZI WA MIZOZO ........ 116
14.0 MATUMIZI YA PESA ........ 125
15.0 MAADILI YA MTU BINAFSI ........ 135
MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA ........ 144
MWONGOZO WA MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI KATIKA GREDI YA SABA ........ 154
MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI ........ 156

## MALENGO YA KITAIFA YA ELIMU NCHINI KENYA

Elimu nchini Kenya inatakiwa:

1. **Kukuza na kustawisha utaifa, uzalendo na kuendeleza umoja wa kitaifa**
   Nchini Kenya kuna jamii zenye mila, dini na tamaduni mbalimbali lakini tofauti hizi hazifai kuzitenganisha. Lazima waweze kuishi na kutangamana kama Wakenya. Elimu ina jukumu kuu la kuwezesha vijana kujenga hisia za uzalendo na utaifa kwa kuondoa mivutano na kukuza mielekeo chanya ya kuheshimiana. Mielekeo hii itawawezesha wanajamii kuishi pamoja kwa utangamano na kujenga uzalendo ili kuchangia ukuaji wa taifa.

2. **Kukidhi mahitaji ya kijamii, kiuchumi, kiteknolojia na viwanda yanayochangia maendeleo ya kitaifa**
   Elimu inafaa kuwaandaa vijana wa taifa la Kenya kutekeleza wajibu wenye umuhimu katika maisha nchini.

   **a) Mahitaji ya kijamii**
   Elimu nchini Kenya lazima iwatayarishe vijana kwa mabadiliko ya mielekeo na mahusiano ambayo yanahitajika kwa maendeleo ya haraka ya uchumi wa kisasa. Kuna uwezekano wa kuwa na mageuzi taratibu ya kijamii kutokana na maendeleo ya haraka ya usasa. Elimu inapaswa kuwasaidia vijana kujirekekebisha kutokana na mabadiliko haya.

   **b) Mahitaji ya kiuchumi**
   Elimu nchini Kenya inafaa kukuza raia walio na stadi, maarifa, ujuzi na sifa za kibinafsi zinazohitajika kuhimili maendeleo ya kiuchumi. Kenya inajenga uchumi huru na wa kisasa ambao unahitaji wafanyakazi wa kutosha, walio na maarifa yanayohitajika humu nchini.

   **c) Mahitaji ya kiteknolojia na ya kiviwanda**
   Elimu nchini Kenya inafaa kuwapa vijana stadi na mielekeo inayohitajika kwa maendeleo ya kiviwanda.
   Kenya inatambua mabadiliko ya haraka ya kiviwanda na kiteknolojia yanayofanyika, hasa katika ulimwengu ulioendelea. Tunaweza kuwa sehemu ya maendeleo haya ikiwa mfumo wetu wa elimu utalenga kimakusudi maarifa, stadi na mielekeo itakayotayarisha vijana kwa mabadiliko ya yanayoendelea ulimwenguni.

3. **Kutoa nafasi ya kujiendeleza na kujitosheleza**
   Elimu inapaswa kuwezesha kutambua, kukuza na kuimarisha vipawa vya kila mmoja ili kuweza kujiendeleza na kujitosheleza. Inafaa kuwawezesha watoto kukuza uwezo wao. Kipengele muhimu cha maendeleo ya kibinafsi ni ujenzi wa tabia ifaayo.

4. **Kuwawezesha wananchi kuimarisha maadili na amali za kijamii na kidini**
   Elimu inakusudiwa kukuza maarifa, stadi na mielekeo itakayoimarisha upataji wa maadili na kuwasaidia watoto kukua wakiwa wenye nidhamu, wanaojitegemea na raia wakamilifu.

5. **Kuimarisha usawa wa kijamii na uwajibikaji**
   Usawa wa kijamii kwa mfano, usawa wa kijinsia huimarika watu wa jamii na jinsia zote wanapopata elimu sawa.
   Elimu inafaa ikuze usawa wa kijamii na uwajibikaji wa kijamii kutokana na mfumo wa elimu unaowezesha fursa sawa ya elimu kwa wote. Inafaa kuwapa watoto wote fursa mbalimbali na zenye changamoto zitakazowawezesha kutoa huduma jumuishi za kijamii bila kujali jinsia, uwezo au mazingira ya kijiografia.

6. **Kukuza uthamini wa tamaduni mbalimbali nchini Kenya**
   Elimu inafaa kuwapa vijana uelewa wa tamaduni za kale na za sasa na nafasi yazo katika jamii ya kisasa. Vijana wanafaa kuambatanisha maadili ya tamaduni bora na mahitaji yanayobadilika kulingana na maendeleo yanayotokea ili kujenga jamii thabiti ya kisasa.

7. **Kuimarisha utambuzi wa uhusiano wa kimataifa na kukuza mwelekeo chanya kwa mataifa mengine**
   Kenya kama nchi mojawapo ya jamii ya kimataifa inakusudia elimu iwaelekeze Wakenya kutambua na kuthamini mahusiano ya kimataifa kwa kuzingatia mikataba, uwajibikaji, haki na manufaa yanayoambatana na ushirika huo.

8. **Kustawisha mwelekeo chanya kuhusu afya bora na uhifadhi wa mazingira**
   Elimu inakusudiwa kujenga mielekeo ifaayo miongoni mwa vijana kuhusu udumishaji wa afya bora na mazingira kwa kujiepusha na mienendo inayoweza kudhuru afya ya mwili na akili. Aidha, inafaa kuimarisha mielekeo chanya kuhusu ukuzaji na uhifadhi wa mazingira na kuwaelekeza vijana kuthamini usafi wa mazingira.

## MGAO WA VIPINDI

| | **Somo** | **Vipindi Kwa Wiki (Dakika 40 kwa kipindi)** |
|---|---|---|
| 1. | English | 5 |
| 2. | Kiswahili/KSL | 4 |
| 3. | Mathematics | 5 |
| 4. | Integrated Science | 5 |
| 5. | Social Studies | 4 |
| 6. | Religious Studies | 4 |
| 7. | Pre-Technical Studies | 4 |
| 8. | Agriculture | 4 |
| 9. | Creative Arts and Sports | 5 |
| | Pastoral/Religious Instructional Programme | 1* |
| **Jumla** | | **40 +1*** |

## MATOKEO YA KIWANGO CHA KATI CHA ELIMU YA MSINGI

Kufikia mwisho wa kiwango cha kati cha elimu mwanafunzi aweze:

1. Kutumia ujuzi wa kusoma na kuandika, ujuzi wa kuhesabu na kufikiri kimantiki ifaavyo katika kujieleza
2. Kuwasiliana kikamilifu katika miktadha mbalimbali
3. Kudhihirisha ujuzi wa kijamii, kiimani na kimaadili kwa ajili ya mahusiano mema
4. Kutalii, kubadilisha, kusimamia na kutunza mazingira ifaavyo kwa ajili ya ujifunzaji na maendeleo endelevu
5. Kufanya usafi, kufuata kanuni zifaazo za usafi na lishe ili kuimarisha afya
6. Kudhihirisha mienendo ya kimaadili na kuonyesha uraia mwema kama wajibu wa kiraia
7. Kuonyesha ridhaa kwa mirathi mingi na tofauti ya kitamaduni nchini ili kuleta mshikamano wa kimahusiano
8. Kudhibiti masuala mtambuko katika jamii ifaavyo
9. Kutumia ujuzi wa kidijitali ifaavyo kwa madhumuni ya mawasiliano na ujifunzaji.

## KAULI KIINI

Somo la Kiswahili litampa mwanafunzi wa Shule ya Junia umilisi katika shughuli za kila siku. Umilisi huu utajengea haiba na uwezo wake wa kuwasiliana na kuhusiana katika jamii, kitaifa na kimataifa. Aidha, litamwendeleza kielimu na kumwandaa kwa ulimwengu wa kazi. Somo hili litampa mwanafunzi hamasa ya kumudu na kufurahia lugha na fasihi kwa kuzihusisha na tajiriba na mazingira yake. Hali kadhalika, litampa mwanafunzi maarifa ya kijamii na kitamaduni. Mwanafunzi ataweza kujieleza na vilevile kupata fursa ya kutoa huduma kwa jamii.

**MATOKEO YA KIJUMLA YANAYOTARAJIWA KATIKA DARAJA LA AWALI LA SHULE ZA UPILI**

Kufikia mwisho wa Shule ya Junia, mwanafunzi aweze:

1. Kujieleza ipasavyo kwa kutumia lugha ya Kiswahili kwa njia ya maandishi na mazungumzo
2. Kuwasiliana ipasavyo katika miktadha mbalimbali ya kijamii
3. Kujenga desturi ya kusoma na kufasiri maandishi kwa ufasaha
4. Kutumia lugha kiubunifu kusimulia na kuandika tungo mbalimbali
5. Kushiriki katika shughuli za kijamii zinazochangia ujifunzaji
6. Kutumia teknolojia ipasavyo katika ujifunzaji na mawasiliano ili kukuza ujuzi wa kidijitali
7. Kutumia maadili yanayohitajika maishani kupitia stadi za lugha ya Kiswahili
8. Kufurahia na kuthamini lugha ya Kiswahili kama lugha rasmi, ya taifa na kimataifa.

## MUHTASARI WA MADA NA MADA NDOGO

| Mada | Mada Ndogo | Idadi ya Vipindi Vilivyopendekezwa |
|---|---|---|
| **Kusikiliza na Kuzungumza** | 1.1.1 Kusikiliza na Kujibu: Mazungumzo | 2 |
| | 2.1.1 Kusikiliza kwa Kina: Sauti /**dh**/ na /**th**/ | 2 |
| | 3.1.1 Tanzu za Fasihi: Fasihi andishi na simulizi | 2 |
| | 4.1.1 Nyimbo: Nyimbo za Watoto na Bembelezi | 2 |
| | 5.1.1 Mazungumzo Mahususi | 2 |
| | 6.1.1 Kusikiliza kwa Kufasiri | 2 |
| | 7.1.1 Kusikiliza kwa Ufahamu: ufahamu wa kusikiliza | 2 |
| | 8.1.1 Kuzungumza ili Kupasha Habari | 2 |
| | 9.1.1 Kusikiliza kwa Kina: Sauti **/d/** na /**nd/** | 2 |
| | 10.1.1 Nyimbo: Nyimbo za Kazi na Nyimbo za Dini | 2 |
| | 11.1.1 Kuzungumza kwa Kuambatanisha na Vitendo/Ishara | 2 |
| | 12.1.1 Kusikiliza kwa Makini | 2 |
| | 13.1.1 Wahusika katika Nyimbo | 2 |
| | 14.1.1 Lugha katika Nyimbo | 2 |
| | 15.1.1 Kusikiliza Habari na Kujibu | 2 |
| **Kusoma** | 1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Kifungu cha Simulizi | 2 |
| | 2.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini ya kujichagulia | 2 |
| | 3.2.1 Kusoma kwa Kina: Novela | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| | 5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu | 2 |
| | 6.2.1 Kusoma kwa Kina: Maudhui na Dhamira | 2 |
| | 7 .2.1 Ufupisho | 2 |
| | 8.2.1 Kusoma kwa Kina: Mandhari na Ploti | 2 |
| | 9.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**:** Kifungu cha Kushawishi | 2 |
| | 10.2.1 Kusoma kwa Kina: Wahusika | 2 |
| | 11.2.1 Kusoma kwa Mapana: Matini ya kujichagulia | 2 |
| | 12.2.1 Kusoma kwa Ufasaha | 2 |
| | 13.2.1 Kusoma kwa Kina: Mbinu za Lugha | 2 |
| | 14.2.1 Kusoma kwa Ufahamu: Kifungu cha Mjadala | 2 |
| | 15.2.1 Ufupisho | 2 |
| **Kuandika** | 1.3.1 Viakifishi: Herufi kubwa na Kikomo | 2 |
| | 2.3.1 Barua ya Kirafiki ya Kutoa Mwaliko | 2 |
| | 3.3.1 Insha za Kubuni | 2 |
| | 4.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |
| | 5.3.1 Insha ya Maelekezo | 2 |
| | 6.3.1 Insha za Kubuni: Picha | 2 |
| | 7.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 8.3.1 Viakifishi: Mabano na Kistari Kifupi | 2 |
| | 9.3.1 Insha za Kubuni: Masimulizi | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 10.3.1 Barua ya Kuomba Msamaha | 2 |
| | 11.3.1 Insha za Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 12.3.1 Hotuba ya Kupasha Habari | 2 |
| | 13.3.1 Insha ya Kubuni: Maelezo | 2 |
| | 14.3.1 Insha ya Maelekezo | 2 |
| | 15.3.1 Kuandika Kidijitali: Baruapepe | 2 |
| **Sarufi** | 1.4.1 Aina za nomino**:** Nomino za Makundi na Nomino za Dhahania | 2 |
| | 2.4.1 Vihusishi: Vihusishi vya **-a** Unganifu na Vihusishi vya Sababu | 2 |
| | 3.4.1 Aina za nomino**:** Nomino za Wingi na Nomino za Vitenzi-jina | 2 |
| | 4.4.1 Nyakati na Hali: Wakati uliopo, Wakati uliopita na Wakati ujao | 2 |
| | 5.4.1 Nyakati na Hali: Wakati uliopita hali ya kuendelea na Wakati ujao hali ya kuendelea | 2 |
| | 6.4.1 Vitenzi**:** Vitenzi Vikuu na Vitenzi Visaidizi | 2 |
| | 7.4.1 Vitenzi Vishirikishi | 2 |
| | 8.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi:<br>Ngeli ya A-WA na Ngeli ya U-I | 2 |
| | 9.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi:<br>Ngeli ya KI-VI na LI-YA | 2 |
| | 10.4.1 Vinyume vya Maneno | 2 |
| | 11.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi: Kauli ya Kutenda, Kutendea na Kutendwa | 2 |

| | | |
|---|---|---|
| | 12.4.1 Aina za Sentensi: Sentensi Sahili | 2 |
| | 13.4.1 Ukanushaji kwa Kuzingatia Nyakati | 2 |
| | 14.4.1 Ukubwa wa Nomino | 2 |
| | 15.4.1 Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa | 2 |
| **Jumla ya vipindi** | | **120** |

**Kumbuka:** Idadi ya vipindi vilivyopendekezwa kwa kila mada ndogo vinaweza kuwa vichache au vingi kutegemea na muktadha.

## MWONGOZO WA KUTUMIA VITABU VYA KUSOMA SHULE YA JUNIA

### Lengo la Vitabu vya Kusoma katika Shule ya Junia

Utanzu ulioteuliwa wa kusomwa katika Gredi ya Saba ni wa Novela. Matokeo yanayotarajiwa:

i. kukuza jadi ya usomaji miongoni mwa wanafunzi jambo ambalo ni muhimu miongoni mwa wanafunzi katika maisha yao ya ujifunzaji,
ii. kuwaandaa wanafunzi kusoma fasihi katika somo la Kiswahili katika mkondo wa Sayansi ya Jamii katika Shule ya Juu,
iii. kuwatanguliza wanafunzi katika vipengele vya kimsingi vya fasihi ambavyo ni muhimu katika maisha ya kila siku tukijua kwamba wengine watasoma fasihi katika Shule ya Juu.

### Kufunza vitabu vya Kusoma katika Shule ya Junia

**Wanafunzi katika shule ya Junia:**

i. wataongozwa kusoma vitabu mbalimbali ili kuwapa nafasi ya kuingiliana na dhana na stadi katika mtaala. Hali hii itawaweka katika hali ya kupata stadi za kuzungumza, kusikiliza, kusoma, kuandika, sarufi mwanzoni,
ii. wanatarajiwa kuingiliana na tanzu mbalimbali ili kuwa na kuwa na uzoevu na dhana za kimsingi za fasihi ili kujiburudisha na pia kukuza mazoea ya usomaji,
iii. hawapaswi kushirikishwa katika uhakiki wa kazi za fasihi kwa undani.

Ni muhimu kukumbuka kuwa ni vitabu tu vilivyoidhinishwa na KICD vinavyopaswa kusomwa kulingana na viwango lengwa.

### Tathmini ya Vitabu vya Kusoma

Kama inavyopendekezwa katika mtaala, tathmini endelevu na tamati haipaswi kuegemea vitabu vyovyote teule. Hii ni kwa sababu vitabu hivi vya kusoma SIO vitabu teule vya fasihi au *setbooks* kama vinavyojulikana. Tathmini inapaswa kuwa wazi na ya vipengele vya kimsingi kulenga dhana za kimsingi kama zinavyoelekezwa katika mtaala. Zaidi ya hayo, tathmini inapaswa kufanywa kwa njia ambayo kila mwanafunzi atakuwa na nafasi sawa bila kujali ni kitabu gani ambacho mwanafunzi amesoma.

## 1.0 USAFI WA KIBINAFSI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **1.1.1 Kusikiliza na Kujibu**<br><br>*Mazungumzo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya kuzingatia katika usikilizaji wa mazungumzo,<br>b) kutambua vipengele vya kuzingatia katika kujibu mazungumzo,<br>c) kutumia vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mazungumzo,<br>d) kuchangamkia kushiriki mazungumzo katika miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mazungumzo,<br>• kutambua vipengele vya kuzingatia katika kujibu mazungumzo,<br>• kusikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa katika kifaa cha kidijitali huku akizingatia vipengele vya kuboresha usikilizaji wa mazungumzo,<br>• kusikiliza na kujibu mazungumzo ipasavyo,<br>• kuigiza mazungumzo (*k.v. ya simu*) kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya kusikiliza na kujibu mazungumzo, | 1. Je, unaposikiliza mazungumzo unapaswa kuzingatia nini ili kupata ujumbe unaowasilishwa?<br>2. Unazingatia nini unapomjibu mtu katika mazungumzo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kushiriki mazungumzo na mzazi au mlezi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya kusikiliza na kujibu mazungumzo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia ipasavyo katika shughuli za ujifunzaji kuhusu kusikiliza na kujibu mazungumzo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia mazungumzo mbalimbali na kutambua vipengele vya kusikiliza na kuzungumza vilivyozingatiwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposikiliza mazungumzo na kuyajibu ipasavyo bila woga. Pia anapochangia katika shughuli ya kikundi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji. Pia anapoheshimu zamu ya wenzake katika mazungumzo.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko:**

- Usafi wa kibinafsi: mwanafunzi anaposikiliza, kushiriki na kuigiza mazungumzo kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza na kujibu mawasiliano aliyojifunza katika somo la Kiwahili na ujifunzaji wa dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa kibinafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.2 Kusoma** | **1.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Simulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha simulizi,<br>b) kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha simulizi,<br>c) kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha simulizi,<br>d) kueleza msamiati katika kifungu cha simulizi,<br>e) kuchangamkia kusoma vifungu vya simulizi ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusoma kifungu cha simulizi kwenye kitabu au kifaa cha kidijitali,<br>• kudondoa habari mahususi (*k.v. nani, nini, wapi, lini*) katika kifungu cha simulizi,<br>• kupanga matukio yanavyofuatana katika kifungu cha simulizi,<br>• kufanya utabiri na ufasiri kutokana na kifungu cha simulizi alichosoma,<br>• kueleza msamiati (*k.v. maneno na nahau*) katika kifungu cha simulizi na kuueleza kwa kutumia kamusi,<br>• kusoma vifungu vya simulizi mtandaoni au kwenye vitabu | 1. Kwa nini tunasoma ufahamu?<br>2. Je, ni mambo gani yanayoweza kukusaidia kuelewa kifungu cha simulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kuhusu suala lengwa (usafi wa kibinafsi) kisha atambue na kueleza maana za msamiati huo kulingana na muktadha wa matumizi,<br>• kumsomea mzazi au mlezi sentensi kuhusu usafi wa kibinafsi kisha kumuelezea maana za msamiati wa suala husika kimuktadha. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kudondoa habari mahususi.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapobashiri na kufasiri kutokana na kifungu cha ufahamu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kusoma vifungu kuhusu suala lengwa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji akiwa na wenzake.

**Masuala Mtambuko:**

- Usafi wa kibinafsi: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa na kuzingatia ujumbe.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha stadi ya kusoma kifungu cha simulizi, na ujifunzaji wa stadi hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa kibinafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.3 Kuandika** | **1.3.1 Viakifishi**<br>• *Herufi kubwa*<br>• *kikomo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua herufi kubwa na kikomo katika matini<br>b) kueleza matumizi ya herufi kubwa na kikomo katika matini,<br>c) kutumia herufi kubwa na kikomo ipasavyo katika matini,<br>d) kuonea fahari matumizi ya herufi kubwa na kikomo katika matini ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua herufi kubwa na kikomo katika maneno, sentensi au vifungu kwenye matini andishi au za kidijitali,<br>• kutafiti mtandaoni au kwenye vitabu vya ziada kuhusu matumizi ya herufi kubwa na kikomo katika maneno, sentensi na vifungu na kuandika daftarini mwake,<br>• kueleza matumizi ya herufi kubwa na kikomo katika maneno, sentensi na vifungu kwenye matini andishi au za kidijitali,<br>• kuandika maneno, sentensi au vifungu vifupi kuhusu suala lengwa kwa kutumia herufi kubwa na kikomo ipasavyo,<br>• kuwasomea wenzake au kuwasambazia kazi yake | Herufi kubwa na kikomo hutumika vipi katika maandishi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwenye mtandao ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasomea wenzake kifungu kwa ufasaha na anaposhiriki katika mijadala na wanafunzi wenzake.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya herufi kubwa na kikomo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti mtandaoni kuhusu matumizi ya herufi kubwa na kikomo katika matini.
- Uwazaji kina: mwanafunzi anapotumia herufi kubwa na kikomo katika kifungu alichokiandika.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
- Usafi wa kibinafsi: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia herufi kubwa na kikomo ipasavyo.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya herufi kubwa na kikomo aliyojifunza katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa kibinafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **1.4 Sarufi** | **1.4.1 Aina za nomino**<br><br>• *Nomino za Pekee na za*<br>• *Kawaida*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za pekee na za kawaida katika matini,<br>b) kutambua aina za nomino za pekee katika matini,<br>c) kutumia nomino za pekee na za kawaida ipasavyo katika matini,<br>d) kuchangamkia matumizi ya nomino za pekee na za kawaida katika matini ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua nomino za pekee na za kawaida kwenye orodha ya maneno, sentensi au vifungu,<br>• kutaja aina za nomino za pekee *(k.v. majina ya watu, siku za wiki, miezi ya mwaka, mito, nchi, anwani za vitabu, za magazeti na za majarida),*<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia nomino za pekee na za kawaida ipasavyo,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia nomino za pekee na za kawaida akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la usafi wa kibinafsi,<br>• kumtajia mzazi au mlezi wake nomino za pekee na za kawaida katika mazingira ya nyumbani. | 1. Ni vitu gani katika mazingira yako ambavyo ni nomino za pekee?<br>2. Ni vitu gani katika mazingira yako ambavyo ni nomino za kawaida? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotaja nomino za pekee na za kawaida akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua nomino za pekee na za kawaida.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino za pekee na za kawaida.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kwa utulivu.

**Masuala Mtambuko:**

Usafi wa kibinafsi: mwanafunzi anapoandika sentensi au kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za pekee na za kawaida.

**Uhusiano na Masomo Mengine**:

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nomino za pekee katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usafi wa kibinafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

## 2.0 LISHE B0RA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **2.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>*Sauti /**dh**/ na /**th**/*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti /**dh**/ na /**th**/ katika silabi na maneno,<br>b) kutamka sauti /**dh**/ na /**th**/ ipasavyo katika silabi na maneno,<br>c) kutumia maneno yenye sauti /**dh**/ na /**th**/ katika sentensi ili kuyatofautisha kimaana,<br>d) kuonea fahari matamshi bora ya sauti /**dh**/ na /**th**/ katika mazungumzo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti **/dh/** na **/th/** katika silabi na maneno,<br>• kutambua maneno yenye sauti **/dh/** na **/th/** yakitamkwa na mwalimu, mgeni mwalikwa au katika kifaa cha kidijitali na kuyatamka ipasavyo,<br>• kutumia maneno yenye sauti **/dh/** na **/th/** kwenye sentensi ili kuyatofautisha kimaana,<br>• kusikiliza sentensi zilizotungwa na wenzake na kutoa maoni yake kuhusu jinsi maneno yenye sauti **/dh/** na **/th/** yalivyotumiwa,<br>• kuunda vitanzandimi vinavyotumia sauti **/dh/** na **/th/** daftarini mwake au kwenye kifaa cha kidijitali, | Ni maneno yepi unayoyajua yaliyo na sauti /**dh**/ na /**th**/? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kusoma vitanzandimi alivyounda akizingatia matamshi bora ya sauti /**dh/** na /**th/** huku wenzake wakisikiliza ili wamtolee maoni,<br>• kumsomea mzazi au mlezi wake kifungu kuhusu suala lengwa akizingatia matamshi bora ya sauti /**dh/** na / **th/**. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kuunda na kusikiliza vitanzandimi vyenye sauti /**dh/** na /**th/**.
- Ubunifu: mwanafunzi anapounda vitanzandimi vyenye maana akitumia maneno yenye sauti /**dh/** na /**th/** na kuvitamka ipasavyo katika kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti /**dh/** na /**th/** katika silabi na maneno na kuunda vitanzandimi kwa kutumia maneno yenye sauti /**dh/** na /**th/**.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na pia kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kwa utulivu.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Lishe bora: mwanafunzi anapotamka na kuzingatia maneno yenye sauti lengwa ipasavyo katika muktadha wa suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya matamshi bora aliyojifunza katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la lishe bora na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.2 Kusoma** | **2.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>• *Matini ya Kujichagulia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza ujumbe wa matini aliyosoma,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia,<br>c) kutumia ipasavyo msamiati uliotumiwa katika matini aliyosoma,<br>d) kujenga mazoea ya kusoma matini za miktadha mbalimbali kupanua mawanda wa fikra. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza ujumbe wa matini aliyoisoma *(andishi au ya kidijitali)*,<br>• kurekodi ujumbe wa matini aliyoisoma katika kijitabu chake kwa marejeleo ya baadaye,<br>• kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia<br>• kutumia kamusi kutafuta maana za maneno asiyoyajua,<br>• kujenga rekodi ya msamiati aliojifunza katika kitabu,<br>• kumtunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma,<br>• kusakura mtandaoni na kujichagulia matini ya ziada kisha aisome na kumweleza | 1. Unapenda kusoma matini za aina gani?<br>2. Unazingatia nini unapochagua matini ya kujisomea? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mzazi au mlezi wake ujumbe wa matini hiyo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika muhtasari na kuuwasilisha kwa wenzake.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kujichagulia matini ya kusoma.

**Maadili:**

- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafuta na kusoma matini aliyojichagulia. Pia anapozingatia nidhamu anaposakura mtandaoni.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza.

**Masuala Mtambuko:**

Lishe bora: mwanafunzi anapotumia ipasavyo msamiati katika matini na kuitumia kutunga sentensi kuhusu lishe bora.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa mapana katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu usomaji huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la lishe bora na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.3 Kuandika** | **2.3.1 Barua ya Kirafiki ya Kutoa Mwaliko**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza umuhimu wa barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko,<br>b) kutambua ujumbe katika barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko,<br>c) kutambua vipengele vya kimuundo vya barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko,<br>d) kuandika barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko kwa kuzingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao,<br>e) kufurahia uandishi wa barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza umuhimu wa kuandika barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko kuhusu masuala mbalimbali,<br>• kutambua ujumbe katika kielelezo cha barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko,<br>• kujadili na wenzake vipengele vya kimuundo vya barua ya kirafiki ya kutoa,<br>• kushiriki katika kujadili na wenzake kuhusu lugha inayofaa katika uandishi wa barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko,<br>• kuandika barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko kuhusu hafla fulani akizingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao na kuwasomea | 1. Je, ni shughuli gani zinazoweza kukufanya uandike barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko?<br>2. Je, ni mambo gani yanayotiliwa maanani katika kuandika barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake darasani ili waitathmini. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kujadili ujumbe, lugha na muundo wa barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko na kuheshimu maoni ya wenzake. Pia anapowasomea wenzake barua aliyoandika.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika kwa mvuto barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko kwa kuzingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapopendekeza shughuli ambazo zinaweza kumfanya aandike barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko. Pia anapoandika barua kuhusu masuala yanayoathiri jamii na kuwashirikisha wenzake katika kupendekeza suluhu.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za kikundi.
- Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kwa utulivu, heshima na kusikilizana.

**Masuala Mtambuko:**

Lishe bora: mwanafunzi anapoandika barua ya kirafiki ya kutoa mwaliko kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa barua ya kirafiki katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la lishe bora na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **2.4 Sarufi** | **2.4.1 Aina za nomino**<br>• *Nomino za Makundi*<br>• *Nomino za Dhahania*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za makundi na za dhahania katika matini,<br>b) kutumia nomino za makundi na za dhahania ifaavyo katika matini,<br>**c)** kuchangamkia kutumia nomino za makundi na za dhahania katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua nomino za makundi na za dhahania kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno na matini nyingine,<br>• kutambua nomino za makundi na za dhahania katika mazingira ya shuleni na nyumbani na kuzitungia sentensi,<br>• kujaza nafasi katika senensi au vifungu kwa kutumia nomino za makundi na za dhahania ifaavyo,<br>• kutunga sentensi au kifungu kifupi kwa kutumia nomino za makundi na za dhahaniaakizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la lishe bora,<br>• kushirikiana na mzazi au mlezi wake kutambua | 1. Ni nomino gani za makundi zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na ya nyumbani?<br>2. Ni nomino gani za dhahania zinazopatikana katika mazingira ya shuleni na ya nyumbani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | nomino za makundi na za dhahania kwenye mtandao au kwenye vitabu vya ziada na kuzitungia sentensi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia kikamilifu katika shughuli za ujifunzaji.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino za makundi na za dhahania.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino za makundi na za dhahania na kuzitungia sentensi na vifungu sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Lishe bora: mwanafunzi anapotunga sentensi na vifungu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nomino za makundi na za dhahania katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu dhana hiyo katika somo la English
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la lishe bora na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

## 3.0 UHURU WA WANYAMA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **3.1.1 Tanzu za Fasihi**<br>• *Fasihi simulizi*<br>• *Fasihi andishi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya fasihi ili kuipambanua,<br>b) kujadili sifa za tanzu za fasihi,<br>c) kutambua aina za tungo za fasihi simulizi na fasihi andishi katika matini,<br>d) kuwasilisha utungo wa fasihi anaoujua,<br>e) kufurahia kushiriki katika uwasilishaji wa fasihi simulizi na fasihi andishi ili kujenga ufasaha wa lugha na fasihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutafiti na kueleza maana ya fasihi katika jamii,<br>● kutambua tanzu za fasihi na kuzitofautisha,<br>● kujadili na wenzake sifa za fasihi simulizi na fasihi andishi,<br>● kutambua tungo za fasihi simulizi na fasihi andishi kutoka simulizi za moja kwa moja au kwenye matini za kidijitali,<br>● kuwasilisha darasani utungo wa fasihi anaoujua *(k.v. hadithi za wanyama)* ili wenzake wausilize na kumtolea maoni,<br>● kushiriki na mzazi au mlezi wake kutafiti kuhusu tanzu | Fasihi inahusika na mambo gani katika jamii? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | za fasihi simulizi na andishi katika jamii yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika kazi ya kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kujifunza sifa za fasihi simulizi na andishi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kutambua tanzu za fasihi simulizi na andishi katika jamii yake.

**Maadili:**
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kujieleza.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uraia: mwanafunzi anapothamini tungo za fasihi simulizi katika jamii.

**Masuala Mtambuko:**
- Uhuru wa wanyama: mwanafunzi anaposimulia tungo na kutilia maanani uhuru wa wanyama.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha tanzu za fasihi simulizi na andishi katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu tanzu hizo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.2 Kusoma** | **3.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>*Novela*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya novela ili kuipambanua,<br>b) kujadili sifa za novela kama utanzu wa fasihi andishi,<br>c) kuchangamkia usomaji wa novela ili kukuza stadi ya kusoma. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutafiti na kueleza maana ya novela,<br>• kutafiti maktabani au mtandaoni kuhusu sifa za novela (*k.v. wahusika wachache na maudhui machache),*<br>• kuwasilisha utafiti wake darasani ili wenzake wamtolee maoni,<br>• kusoma novela iliyoteuliwa na mwalimu na kutambua sifa zake,<br>• kumsomea mzazi au mlezi sifa za novela aliyosoma. | Unawezaje kutofautisha novela na tungo nyingine za fasihi andishi? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa**:

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia katika shughuli za kikundi kwa kutumia lugha fasaha.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti maktabani au mtandaoni kuhusu maana na sifa za novela. Pia anaposoma tafiti za wenzake na kuzitolea maoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake utafiti wake kuhusu sifa za novela.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kikundi wanapojadili sifa za novela.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali ipasavyo na kuzingatia maadili anapotafiti mtandaoni.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kuwasilisha maoni yao kuhusu utafiti wake wa sifa za novela. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai kulingana na maudhui yaliyoangaziwa katika novela. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha usomaji wa novela katika somo la Kiswahili na yale amejifunza kuhusu usomaji huo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.3 Kuandika** | **3.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kuteua mada na ujumbe wa kuandikia insha ya kubuni,<br>b) kujadili vidokezo kulingana na mada ya kuandikia insha ya kubuni,<br>c) kuandika vidokezo vyenye ujumbe unaolingana na mada ya insha ya kubuni,<br>d) kuandika insha ya kubuni inayozingatia vidokezo vilivyoandaliwa,<br>e) kufurahia kuandaa vidokezo vyenye ujumbe unaolingana na mada ya insha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kuteua mada anayoweza kuiandikia insha ya kubuni<br>● kuteua ujumbe unaoafiki mada aliyoiteua,<br>● kujadiliana na wenzake vidokezo vya mada aliyoteua,<br>● kuandika vidokezo vyenye ujumbe unaolingana na mada,<br>● kuandika insha ya kubuni inayozingatia vidokezo alivyoandaa,<br>● kuwasilisha insha yake darasani au mtandaoni ili wenzake wamtolee maoni. | Ni mambo gani unayozingatia unapoandaa vidokezo vya insha ya kubuni? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kwa ufasaha vidokezo vya insha ya kubuni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoteua mada na vidokezo mwafaka vya kuandikia insha ya kubuni.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti kuhusu mada anayoandikia insha ya kubuni kwenye makala mbalimbali.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuteua mada mwafaka na kuiandalia vidokezo.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi. Pia anapozingatia nidhamu anaposakura mtandaoni.

**Masuala Mtambuko:**

Elimu ya utunzaji wa wanyama: mwanafunzi anapotafiti na kuteua mada kuhusu masuala yanayoathiri jamii.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya kubuni katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **3.4 Sarufi** | **3.4.1 Aina za nomino**<br><br>• *Nomino za Wingi*<br>• *Nomino za Vitenzi-jina*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino za wingi na za vitenzi-jina katika matini,<br>b) kutumia nomino za wingi na za vitenzi-jina ipasavyo katika matini,<br>c) kufurahia matumizi ya nomino za wingi na za vitenzi-jina katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua nomino za wingi na za vitenzi-jina kwenye chati, kadi maneno au kapu maneno,<br>● kutenga nomino za wingi na za vitenzi-jina katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino katika matini za kidijitali,<br>● kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia nomino za wingi na za vitenzi-jina ipasavyo,<br>● kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia nomino za wingi na za vitenzi-jina akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la uhuru wa wanyama,<br>● kushirikiana na mzazi au mlezi wake kutafiti *(k.v. mtandaoni na vitabuni)* kuhusu nomino za wingi na za vitenzi-jina na kuzitungia sentensi kisha awasomee wenzake darasani ili wamtolee maoni. | Je, ni nomino zipi za wingi na za vitenzi jina zinazopatikana katika mazingira yako? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia katika kazi za kikundi kutambua na kutenga nomino za wingi na za vitenzi-jina.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino za wingi na za vitenzi-jina.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua nomino za wingi na za vitenzi-jina na kuzitungia sentensi na vifungu sahihi. |
| **Maadili:**<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Maslahi ya wanyama: mwanafunzi anapotunga aya na sentensi kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za wingi na za vitenzi-jina. |
| **Uhusiano na Masomo Mengin:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nomino katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utunzaji wa wanyama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Agriculture. |

## 4.0 AINA ZA MALIASILI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **4.1.1 Nyimbo**<br><br>• *Nyimbo za*<br>• *Watoto Bembelezi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya nyimbo za watoto na bembelezi,<br>b) kujadili sifa za nyimbo za watoto na bembelezi,<br>c) kujadili mitindo ya uwasilishaji wa nyimbo za watoto na bembelezi,<br>d) kuwasilisha nyimbo za watoto na bembelezi kwa kuzingatia uwasilishaji ufaao,<br>e) kuchangamkia uwasilishaji wa | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya nyimbo za watoto na bembelezi,<br>• kutafiti vitabuni au mtandaoni kuhusu sifa za nyimbo za watoto na bembelezi,<br>• kuwasilisha matokeo ya utafiti wake kwa wenzake ili waweze kujadili sifa hizo,<br>• kusikiliza nyimbo za watoto na bembelezi kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>• kushirikiana na wenzake kujadili mitindo ya uwasilishaji wa nyimbo za watoto na bembelezi *(k.v. urudiaji wa sauti, maneno na vifungu vya maneno, uchezeshaji wa* | 1. Je, ni nyimbo gani za watoto unazozijua katika jamii yako?<br>2. Unapomwimbia mtoto bembelezi, unazingatia nini ili apate kulala? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | nyimbo za watoto na bembelezi ili kukuza ubunifu. | *viungo vya mwili,)* katika nyimbo walizosikiliza,<br>● kuimba nyimbo za watoto na bembelezi kwa kuzingatia mitindo mbalimbali ya uwasilishaji,<br>● kutunga nyimbo nyepesi za watoto na bembelezi na kuziwasilisha kwa kutumia mitindo ifaayo,<br>● kuimba wimbo wa watoto na bembelezi akiwa na mzazi au mlezi wake na kujadili ujumbe katika nyimbo hizo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza nyimbo mbalimbali za watoto na bembelezi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoimba na kuwasilisha nyimbo. Pia anapochangia ifaavyo katika shughuli za kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kuimba nyimbo za watoto na bembelezi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Haki za watoto: mwanafunzi anapotunga na kuwasilisha nyimbo zinazohusu masuala ya watoto. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nyimbo katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English na Creative Arts and Sports.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la aina za maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.2 Kusoma** | **4.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>b) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>c) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>d) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>e) kuridhia kusoma makala kwa kuzingatia vipengele vinavyofanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha,<br>● kutazama vielelezo vya video za watu wanaosoma makala *(k.v. hotuba na habari)* kwa ufasaha,<br>● kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali akizingatia matamshi bora,<br>● kusoma kifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno sahihi yasiyopungua 90 kwa dakika*),<br>● kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo *(k.v. kiwango cha sauti na kiimbo),*<br>● kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo panapofaa *(k.v. ishara za uso na mikono),* | Unazingatia nini ili kusoma makala kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kusoma mbele ya wenzake kazi yake ili wamtolee maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi makala akizingatia vipengele vya usomaji bora. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapofanikiwa kusoma makala kwa ufasaha na anapojadiliana na wenzake katika kikundi kuhusu vipengele vya kimsingi vya kusoma kwa ufasaha.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa ufasaha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia ishara zifaazo wakati wa kusoma kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kusoma anakuza hamu ya ujifunzaji.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi wanapojadili vipengele vya usomaji bora.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika mjadala wakati wa shughuli ya ujifunzaji katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuwasomea wenzake kifungu.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi kujadili vipengele vya usomaji bora.

**Masuala Mtambuko:**

- Masuala ya elimu ya mazingira: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu maliasili.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufasaha katika somo la Kiswahili na usomaji huo katika somo la English.Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la aina za maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.3 Kuandika** | **4.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua lugha ya kiubunifu katika insha za masimulizi,<br>b) kujadili umuhimu wa lugha ya kiubunifu katika insha za masimulizi,<br>c) kubainisha wahusika na mandhari katika insha za masimulizi,<br>d) kujadili umuhimu wa wahusika na mandhari katika insha za masimulizi,<br>e) kuandika insha ya masimulizi akizingatia lugha, wahusika na mandhari ifaavyo,<br>f) kufurahia kuandika insha ya masimulizi akizingatia lugha, wahusika na | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua lugha ya kiubunifu katika vielelezo vya insha za masimulizi,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa lugha ya kiubunifu katika vielelezo vya insha za masimulizi,<br>● kubainisha wahusika na mandhari katika vielelezo vya insha za masimulizi kutoka kwenye maandishi au vifaa vya kidijitali,<br>● kushirikiana na wenzake kujadili umuhimu wa wahusika na mandhari katika insha za masimulizi,<br>● kuandika insha ya masimulizi akitumia lugha kiubunifu na kuwabainisha wahusika na mandhari akizingatia suala lengwa, | Je, ni mambo gani utahitaji kuzingatia ili kuandika insha nzuri ya masimulizi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | mandhari ifaavyo ili kukuza ubunifu. | ● kuwasomea wenzake insha aliyoandika ili waitathmini,<br>● kumsomea mzazi au mlezi kielelezo cha insha ya masimulizi kisha atambue matumizi ya lugha kiubunifu na ubainishaji wa wahusika na mandhari. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadili kwa ufasaha umuhimu wa ubainishaji wa wahusika na mandhari katika insha za masimulizi. Pia anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waitathmini.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha kwa kutumia lugha kiubunifu na kubainisha wahusika na mandhari.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha ya masimulizi.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi. Pia anapotathmini insha za wenzake.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya elimu ya mazingira: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi kuhusu aina za maliasili kwa kuzingatia matumizi ya lugha kiubunifu, ubainishaji wa wahusika na mandhari.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la aina za maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **4.4 Sarufi** | **4.4.1 Nyakati na Hali;**<br><br>• *Wakati uliopo*<br>• *Wakati uliopita*<br>• *Wakati ujao*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kubainisha vitenzi vilivyo katika wakati uliopo, uliopita na ujao katika matini,<br>b) kutumia wakati uliopo, uliopita na ujao ifaavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia wakati uliopo, uliopita na ujao ifaavyo ili kuboresha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kubainisha vitenzi vilivyo katika wakati uliopo, uliopita na ujao kutoka kwenye chati, mti maneno, kapu maneno au kwa kuvipigia mstari kwenye sentensi na vifungu,<br>• kusoma kifungu na kutambua nyakati zilizotumiwa,<br>• kubadilisha nyakati katika sentensi au vifungu kulingana na maagizo,<br>• Kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia wakati uliopo, uliopita na ujao ipasavyo<br>• kuandika sentensi au vifungu vifupi katika wakati uliopo, uliopita au ujao daftarini mwake au kwenye kifaa cha kidijitali akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la aina za maliasili,<br>• kuwasomea wenzake au kuwasambazia kazi yake mtandaoni ili waitolee maoni, | Kwa nini tunatumia nyakati mbalimbali katika mawasiliano? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowatungia wenzake sentensi kwa kutumia wakati uliopo, uliopita na ujao ifaavyo. Pia anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika kazi za kikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika sentensi katika wakati lengwa na kuwasambazia wenzake mtandaoni.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi na kuzibadilisha katika wakati uliopo, uliopita na ujao ipasavyo.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapochangia kutambua nyakati na kuzitungia sentensi ifaavyo. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi. Pia anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya elimu ya mazingira: mwanafunzi anapotunga sentensi na vifungu mbalimbali kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nyakati na hali katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la aina za maliasili na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

## 5.0 UNYANYASAJI WA KIJINSIA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **5.1.1 Mazungumzo Mahususi**<br><br>• *Maamkuzi*<br>• *Maagano*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali za siku,<br>b) kutambua majibu ya maamkuzi na maagano ya nyakati mbalimbali za siku,<br>c) kutambua maamkuzi yanayotumiwa na makundi mbalimbali ya kijamii pamoja na majibu ya maamkuzi hayo,<br>d) kutumia maamkuzi na maagano mwafaka katika miktadha mbalimbali, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua, katika mazungumzo, kapu maneno, kadi maneno au matini mbalimbali, maamkuzi pamoja na majibu ya maamkuzi hayo *(k.v. habari za asubuhi: njema/nzuri, sabalkheri: aheri)* na maagano pamoja na majibu ya maagano hayo *(k.v. kwaheri: ya kuonana, alamsiki: binuru)* yanayotumiwa katika miktadha anuwai,<br>• kutambua maamkuzi mwafaka kwa kuzingatia mahusiano ya kijamii na | 1. Je, ni maamkuzi na maagano gani yanayotumiwa katika jamii yako?<br>2. Kwa nini ni muhimu kujua maamkuzi na maagano mbalimbali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kujenga mazoea ya kutumia maamkuzi na maagano mwafaka katika maisha ya kila siku ili kufanikisha mahusiano. | maagano mwafaka kulingana na nyakati za siku,<br>● kusikiliza mazungumzo kuhusu suala lengwa katika kifaa cha kidijitali na kutaja maamkuzi na maagano yaliyotumiwa,<br>● kuigiza mazungumzo kwa kuzingatia maamkuzi na maagano mwafaka,<br>● kushiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake kwa kuzingatia maamkuzi na maagano mwafaka. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoigiza mazungumzo na wenzake kwa kuzingatia maamkuzi na maagano yafaayo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza maamkuzi na maagano mbalimbali.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na kutumia maamkuzi na maagano kwa ukakamavu.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anaposhiriki katika uigizaji na anapotunza vifaa vya kidijitali vinavyotumiwa.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Masuala ya kijamii: mwanafunzi anapotumia maamkuzi na maagano ifaayo akizingatia umri, cheo au rika. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maamkuzi na maagano katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la unyanyasaji wa kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.2 Kusoma** | **5.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu,<br>b) kueleza habari za kifungu cha ufahamu kwa ufupi,<br>c) kueleza maana ya msamiati kulingana na muktadha wa kifungu cha ufahamu,<br>d) kuchangamkia kusoma kwa ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kudondoa habari mahususi *(k.v. nani, nini, wapi, lini)* katika kifungu cha ufahamu,<br>• kutambua msamiati wa suala lengwa katika kifungu cha ufahamu na kuueleza kwa kutumia kamusi,<br>• kuandika habari za kifungu cha ufahamu kwa ufupi,<br>• kuwawasilishia wenzake kazi yake ili wamtolee maoni,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu cha ufahamu na kisha kujibu maswali. | Unazingatia nini unapodondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma kifungu.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kusoma na kudondoa habari katika kifungu.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposoma kwa ufasaha na kubainisha ujumbe katika kifungu na kukiandika kwa ufupi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposakura na kusoma makala mbalimbali ya suala lengwa ili kusoma vifungu.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Masuala ya kijinsia: mwanafunzi anaposoma matini kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufahamu katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la unyanyasaji wa kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.3 Kuandika** | **5.3.1 Insha ya Maelekezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya insha ya maelekezo,<br>b) kutambua aina za insha za maelekezo,<br>c) kujadili sifa za insha ya maelekezo,<br>d) kuandaa mpangilio wa hatua za insha ya maelekezo,<br>e) kuandika insha ya maelekezo akizingatia vipengele muhimu vya insha ya maelekezo,<br>f) kufurahia kuandika insha ya maelekezo akizingatia vipengele vyake muhimu ili | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutafiti na kueleza maana ya insha ya maelekezo,<br>● kutambua anwani ya insha ya maelekezo ambayo amesoma kwenye matini,<br>● kutambua aina za insha za maelekezo kwenye maandishi au vifaa vya kidijitali,<br>● kujadili na wenzake sifa za insha ya maelekezo kwa kuzingatia vielelezo vya insha kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali,<br>● kushiriki katika kikundi kuandaa mpangilio ufaao wa hatua za insha ya maelekezo,<br>● kuandika insha ya maelekezo akizingatia vipengele vyake muhimu (*k.v. anwani na mpangilio mwafaka wa hatua*) huku akitumia vipengele vya | Ukimwelekeza rafiki yako nyumbani kwenu utatumia mpangilio gani wa hatua ili asipotee njia? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kufanikisha mawasiliano. | lugha vinavyotumiwa kuelekeza ili kumjengea msomaji taswira kamili ya anachoelekezwa kufanya,<br>● kuwasomea wenzake katika kikundi insha aliyoandika darasani au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni,<br>● kuandika insha ya maelekezo akizingatia anwani na mpangilio mwafaka wa hatua huku akitumia vipengele vya lugha vinavyotumiwa kuelekeza ili kumjengea msomaji taswira kamili ya anachoelekezwa kufanya,<br>● kuwasomea wenzake katika kikundi insha aliyoandika darasani au kuwasambazia kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika insha kwa ufasaha na anapoisoma vizuri. Pia anaposhiriki na wenzake katika kujadili kuhusu insha ya maelekezo.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoteua lugha mwafaka na kufaulu kutoa maelezo bayana ya anachoelekeza.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha hadharani. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya kijamii: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala la kijinsia. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelekezo katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la unyanyasaji wa kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **5.4 Sarufi** | **5.4.1 Nyakati na Hali**<br>• *Wakati uliopita hali ya kuendelea*<br>• *Wakati ujao hali ya kuendelea*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kubainisha vitenzi vilivyo katika wakati uliopita hali ya kuendelea na ujao hali ya kuendelea katika matini,<br>b) kutumia wakati uliopita hali ya kuendelea na ujao hali ya kuendelea ifaavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia wakati uliopita hali ya kuendelea na ujao hali ya kuendelea ifaavyo ili kuboresha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kubainisha vitenzi vilivyo katika wakati uliopita hali ya kuendelea na ujao hali ya kuendelea kutoka kwenye chati, mti maneno, kapu maneno au kwa kuvipigia mstari kwenye sentensi na vifungu,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa na kutambua nyakati na hali zilizotumiwa,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia wakati uliopita hali ya kuendelea na ujao hali ya kuendelea ifaavyo akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la unyanyasaji wa kijinsia,<br>• kuandika sentensi kuhusu suala lengwa katika wakati uliopita hali ya kuendelea na ujao hali ya kuendelea kwenye kifaa cha kidijitali na kuwasambazia wenzake mtandaoni ili waziweke katika nyakati na hali zinazozingatiwa, | Kwa nini tunazingatia nyakati na hali mbalimbali katika mawasiliano? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kubadilisha nyakati na hali katika kifungu kulingana na maagizo. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kuandika sentensi katika wakati na hali lengwa na kuwasambazia wenzake mtandaoni.
- Ubunifu: mwanafunzi anapobadilisha nyakati na hali mbalimbali na kutunga sentensi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapochangia kutambua nyakati na hali na kuzitungia sentensi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kubadilisha nyakati na hali katika kifungu.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Masuala ya kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala la kijinsia.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya wakati uliopita hali ya kuendelea na ujao hali ya kuendelea katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la unyanyasaji wa kijinsia na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

SNK Educational Consulting

## 6.0 USALAMA SHULENI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **6.1.1 Kusikiliza kwa Kufasiri**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza kwa usahihi masuala yanayozungumziwa katika matini ya kusikiliza,<br>b) kufasiri habari katika matini ya kusikiliza,<br>c) kueleza maana ya msamiati kama ulivyotumika katika matini ya kusikiliza,<br>d) kutabiri kitakachotokea katika matini kwa kurejelea vidokezo katika matini ya kusikiliza, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusikiliza matini kuhusu suala lengwa ( kama vile visababishi vya ajali shuleni,mbinu za kupunguza ajali za barabarani)<br>• kufasiri habari katika matini aliyosikiliza,<br>• kueleza maana ya msamiati wa suala lengwa kama ulivyotumika katika habari aliyosikiliza,<br>• kutabiri kitakachotokea katika matini kwa kurejelea vidokezo *(k.v. picha, kichwa/anwani na toni ya mzungumzaji)* vilivyopo katika matini, | Je, ni mambo gani utakayozingatia katika kuchanganua habari uliyosikiliza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kufurahia kufasiri matini za kusikiliza ili kukuza stadi ya kusikiliza. | • kushirikiana na mzazi au mlezi kusikiliza na kuchanganua habari katika matini za aina mbalimbali kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoeleza kwa ufasaha masuala yanayozungumziwa katika matini aliyosikiliza.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia ipasavyo vifaa vya kidijitali kama vile simu, redio, kipakatalishi au runinga kusikiliza matini.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapotabiri kitakachotokea katika matini aliyosikiliza.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Suala la usalama: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kikundi kuchanganua habari kwenye matini aliyosikiliza kuhusu usalama shuleni.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa kufasiri katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports, Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.2 Kusoma** | **6.2.1 Kusoma kwa Kina** Novela<br>-*Maudhui*<br>-*Dhamira*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza dhana za maudhui na dhamira katika fasihi,<br>b) kujadili maudhui katika novela,<br>c) kujadili dhamira katika novela,<br>d) kutoa muhtasari wa dhamira na maudhui kuhusu novella,<br>e) kujenga mazoea ya usomaji wa kazi za fasihi katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya maudhui katika fasihi,<br>● kutambua maudhui mbalimbali katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kujadili maudhui ya novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu maudhui ili waitolee maoni,<br>● kuandika maelezo mafupi kuhusu maudhui katika novela aliyosoma,<br>● kushirikiana na mzazi au mlezi kusoma chapisho la novela au kutoka mtandaoni na kutambua ujumbe wake,<br>● kueleza maana ya dhamira katika fasihi,<br>● kutambua dhamira ya novela iliyoteuliwa na mwalimu , | Vitabu vya fasihi ulivyowahi kusoma vinazungumzia nini? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kuandika maelezo mafupi kuhusu dhamira ya novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu dhamira,<br>● kumsomea mzazi au mlezi novela iliyochapishwa au kutoka mtandaoni na kutambua dhamira yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji kuhusu maudhui na dhamira kwenye novela akiwa na wenzake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake ufupisho wa maudhui na dhamira ili waujadili na kutoa maoni.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapochambua maudhui na dhamira katika novela na kushirikiana na mzazi au mlezi katika uchambuzi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapotambua na kujadili maudhui na dhamira kwenye novela katika kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kuhusu uwasilishaji wa wengine ili kuwarekebisha na kuwahimiza.
- Umoja: mwanafunzi anapotagusana na wengine katika kikundi ili kutambua na kujadili maudhui na dhamira kwenye novela.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai kulingana na maudhui yaliyoangaziwa katika novela. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya maudhui na dhamira katika novela katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports, Integrated Science na Agriculture. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.3 Kuandika** | **6.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>Picha<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kubuni anwani inayooana na kisa atakachosimulia kutokana na picha katika matini,<br>b) kutoa maelezo dhahiri kuhusu matukio katika picha kwenye matini,<br>c) kuandika kisa chenye maelezo dhahiri kutokana na picha katika matini,<br>d) kufurahia kusimulia kisa kutokana na picha ili kukuza ubunifu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusimuliana matukio kutokana na picha kwenye matini kuhusu suala lengwa,<br>● kubuni anwani inayooana na kisa atakachosimulia kutokana na picha kwenye matini,<br>● kutoa maelezo dhahiri kuhusu matukio katika picha kwenye matini,<br>● kuandika kisa chenye maelezo dhahiri kutokana na picha kwenye matini,<br>● kuwasomea wenzake kisa alichoandika ili wakitolee maoni,<br>● kushirikiana na mzazi au mlezi wake kutafiti mtandaoni au vitabuni kuhusu insha za picha kisha wasimuliane visa kutokana na picha. | Je, ni vigezo vipi utakavyozingatia wakati wa kuandika insha ya kubuni kutokana na picha? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kujadiliana kuhusu matukio kwenye picha na kutoa maelezo dhahiri kutokana na picha hizo.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia kifaa cha kidijitali kutafiti kuhusu insha za kusimulia mtandaoni.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika kisa chenye maelezo dhahiri kutokana na picha.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafuta habari mtandaoni au vitabuni na mzazi au mlezi wake. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu usalama shuleni. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya picha katika katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports, Integrated Science na Agriculture. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **6.4 Sarufi** | **6.4.1 Vitenzi**<br>• *Vitenzi Vikuu*<br>• *Vitenzi Visaidizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi vikuu na visaidizi katika matini,<br>b) kutumia vitenzi vikuu na visaidizi ipasavyo katika matini,<br>c) kuchangamkia kutumia vitenzi vikuu na visaidizi ipasavyo katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vitenzi vikuu *(k.v. alikuwa <u>anacheka</u>, angali <u>anasoma)</u>* na visaidizi *(k.v. kuwa, weza, kuja, -ngali, bidi na wahi)* kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>● kubainisha vitenzi vikuu na visaidizi katika sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi au chati kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari,<br>● kutunga sentensi akitumia vitenzi vikuu na visaidizi ipasavyo kwa kuzingatia masuala mtambuko anuwai likiwemo suala la usalama shulen,<br>● kutunga sentensi zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani kwa kutumia vitenzi vikuu na visaidizi *(k.v. Mtoto huyu **huwa anajali** usalama wake).* | Tunatofautisha vitenzi vikuu na vitenzi visaidizi kwa njia gani? |

| |
|---|
| **iUmilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapochangia kazi za kikundi huku akiwapa wenzake nafasi ya kushiriki na kutoa maoni yao.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vitenzi vikuu na visaidizi.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi akitumia vitenzi vikuu na visaidizi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapochangia kutambua vitenzi vikuu na visaidizi na kuvitungia sentensi na vifungu sahihi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kutunga sentensi zenye vitenzi vikuu na visaidizi vinavyohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wengine nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake na kuchangia katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Usalama shuleni: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu usalama kwa kutumia vitenzi vikuu na visaidizi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vitenzi vikuu na visaidizi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la usalama na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Creative Arts and Sports, Integrated Science na Agriculture. |

## 7.0 KUHUDUMIA JAMII SHULENI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **7.1.1 Kusikiliza kwa Ufahamu**<br><br>*Ufahamu wa kusikiliza*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe katika ufahamu wa kusikiliza,<br>b) kueleza maana ya msamiati ulio katika ufahamu wa kusikiliza,<br>c) kufasiri ujumbe kutokana na ufahamu wa kusikiliza,<br>d) kuchangamkia kushiriki katika kusikiliza kwa ufahamu ili kukuza stadi ya kusikiliza kwa ufahamu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua ujumbe wa suala lengwa uliotumiwa katika ufahamu wa kusikiliza kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye kifaa cha kidijitali,<br>• kueleza maana za msamiati wa suala lengwa kama ulivyotumiwa katika kauli au sentensi zilizosemwa,<br>• kusikiliza kauli au vifungu vya sentensi kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu au mgeni mwalikwa na kufasiri ujumbe katika kauli au sentensi hizo, | Je, kusikiliza kwa ufahamu kuna faida zipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kushirikiana na mzazi au mlezi kusikiliza ufahamu kuhusu suala lengwa kutoka kwa kifaa cha kidijitali na kutambua maana ya msamiati na ujumbe muhimu. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kujadili kuhusu vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza kwa ufahamu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikiliza kauli na sentensi na kujibu.
- Ubunifu: mwanafunzi anaposikiliza na kusema upya alichoambiwa. Pia anapofasiri wazo kuu.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapofasiri ujumbe kutokana na ufahamu wa kusikiliza.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi. Pia anapoheshimu zamu ya wenzake katika mazungumzo.
- Upendo: mwanafunzi anapowasikiliza wasemaji kwa makini. Pia anapowapa wanafunzi wenzake zamu ya kuzungumza.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Mshikamanano wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya ujifunzaji wa kusikiliza kwa ufahamu kuhusu kuhudumia jamii shuleni.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa ufahamu katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika jamii shuleni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

SNK Educational Consulting

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.2 Kusoma** | **7.2.1 Ufupisho**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ufupisho ili kuupambanua,<br>b) kutambua habari kuu za aya na kuzieleza kwa usahihi katika sentensi moja,<br>c) kufupisha kifungu akizingatia mpangilio ufaao wa habari kutokana na matini,<br>d) kufurahia kufupisha habari kwa usahihi katika mawasiliano ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya ufupisho,<br>• kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali,<br>• kutambua kwenye matini andishi au ya kidijitali habari kuu za aya na kuzieleza kwa usahihi kwa kuzingatia mtazamo wa matini katika matini ya kufupishwa akishirikiana na wenzake,<br>• kufupisha kifungu alichosoma kwa kuzingatia mpangilio ufaao wa habari sahihi kutokana na matini,<br>• kuwawasilishia wenzake kazi yake ili waitolee maoni. | Unazingatia nini unapofupisha kifungu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake katika kikundi habari kuu za aya kwenye kifungu alichosoma.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapoandaa ufupisho na kuwawasilishia wenzake ili waitolee maoni.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika ufupisho kwa kuzingatia mpangilio ufaao.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposoma kifungu mtandaoni na kudondoa hoja muhimu. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi wanapojadili hoja na maneno muhimu.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi. Pia, anapojitolea kuiandaa kazi yake ili kuwawasilishia wenzake.<br>• Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi kujadili maneno na hoja muhimu katika kifungu. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Uongozi na utawala mwema: mwanafunzi anapofupisha kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufupisho katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika jamii shuleni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.3 Kuandika** | **7.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya insha ya maelezo,<br>b) kutambua msamiati ufaao katika kutoa maelezo,<br>c) kutambua umuhimu wa msamiati ufaao katika insha ya maelezo,<br>d) kutumia msamiati ufaao kwa ufasaha katika kuandika insha ya maelezo,<br>e) kufurahia kuandika insha za maelezo ili kujenga stadi ya kuandika. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua msamiati ufaao katika kutoa maelezo *(k.v. vivumishi na vielezi)* kutoka kwa vielelezo vya insha kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali ,<br>• kutumia kifaa cha kidijitali kupigia mstari maneno yaliyotumiwa kutoa maelezo katika kifungu,<br>• kutambua umuhimu wa kuteua maneno yafaayo katika kielelezo cha insha ya maelezo,<br>• kuandika insha ya maelezo kwa kuzingatia msamiati ufaao ili kujenga maelezo dhahiri yenye kuathiri hisia mbalimbali na kutekeleza majukumu ya kushawishi, kuburudisha, kupasha habari au kufunza,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni. | Je, unatumia lugha ya aina gani unapotaka kumweleza mtu jambo fulani ili aweze kupata picha kamili? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusahihisha insha.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kupigia mstari maneno yaliyotumiwa kutoa maelezo katika kifungu.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapofaulu kuandika insha inayosawiri picha halisi ya kitu anachoelezea.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Haki na majukumu ya kibinadamu:mwanafunzi atakapoandika insha ya maelezo akizingatia suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika jamii shuleni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **7.4 Sarufi** | **7.4.1 Vitenzi Vishirikishi**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vitenzi vishirikishi katika matini,<br>b) kutumia vitenzi vishirikishi katika matini,<br>c) kuonea fahari matumizi ya vitenzi vishirikishi katika sentensi na vifungu. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kujadili na mwenzake maana ya vitenzi vishirikishi,<br>• kuchopoa vitenzi vishirikishi (*k.v. ni, si, yu, ndiye, ndio, ndipo*) kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>• kutaja vitenzi vishirikishi vinavyojitokeza katika sentensi na vifungu,<br>• kutenga vitenzi vishirikishi katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi kwa kuvikolezea wino au kuvipigia mstari,<br>• kutunga sentensi na vifungu kwa kutumia vitenzi vishirikishiakizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la kuhudumia jamii shuleni,<br>• kutunga sentensi zenye vitenzi vishirikishi zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani na kumsomea mzazi au mlezi wake *(k.v. mimi ni mwanafunzi mtiifu).* | Je, unajua aina gani za vitenzi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotaja kwa uwazi vitenzi vishirikishi vinavyojitokeza katika sentensi na vifungu. Pia anapojadiliana na mwenzake kuhusu maana ya kitenzi kishirikishi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua vitenzi vishirikishi.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vitenzi vishirikishi.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki kutambua vitenzi vishirikishi na kuvitungia sentensi sahihi na vifungu kwa ukakamavu. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala ya huduma kwa jamii: mwanafunzi anapoandika sentensi na vifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia vitenzi vishirikishi. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vitenzi vishirikishi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la huduma katika jamii shuleni na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

## 8.0 ULAGUZI WA BINADAMU

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **8.1.1 Kuzungumza ili Kupasha Habari**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kuzungumza ili kupasha habari ili kutofautisha na aina nyingine za uzungumzaji,<br>b) kutambua aina za uzungumzaji wa kupasha habari,<br>c) kujadili vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza ili kupasha habari,<br>d) kupasha habari kwa kutumia vipengele vifaavyo, | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya kuzungumza ili kupasha habari,<br>• kujadili na wenzake aina za uzungumzaji wa kupasha habari katika jamii yake,<br>• kusikiliza aina mbalimbali za uzungumzaji kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa, wanafunzi wenzake au vifaa vya kidijitali,<br>• kutambua uzungumzaji wa kupasha habari kutoka kwenye aina za uzungumzaji alizosikiliza,<br>• kujadili vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza ili kupasha habari,<br>• kusikiliza uzungumzaji wa kupasha habari ukitolewa na | 1. Je, uzungumzaji wa kupasha habari hutolewa katika miktadha gani ya jamii yako?<br>2. Je, utatumia mikakati gani ili kuwapasha wanajamii habari kuhusu mambo mbalimbali? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | e) kuchangamkia kupasha habari mbalimbali ili kufanikisha mawasiliano. | mwalimu, mgeni mwalikwa au katika vifaa vya kidijitali na kutathmini kama umetumia vipengele vifaavyo vya kuzungumza ili kupasha habari,<br>• kushiriki katika uzungumzaji wa kupasha habari kuhusu suala lengwa akitumia vipengele vifaavyo vya mazungumzo ya kupasha habari,<br>• kushiriki katika mazungumzo na mzazi au mlezi wake kuhusu suala lengwa huku akitumia vipengele vifaavyo vya kupasha habari. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kikundi kujadili aina za uzungumzaji wa kupasha habari katika jamii yake. Pia anapowaeleza wenzake kuhusu vipengele vya kuzingatia ili kufanikisha mawasiliano.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga uzungumzaji ili kupasha habari kuhusu suala lengwa.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki katika uzungumzaji ili kupasha habari kuhusu suala lengwa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki na mzazi au mlezi wake katika uzungumzaji ili kupasha habari kuhusu suala lengwa.

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za ujifunzaji.<br>• Upendo: mwanafunzi anapoihusisha hadhira yake. Pia anapowapa wenzake zamu ya kushiriki katika mazungumzo kuhusu suala lengwa.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika kujifunza uzungumzaji ili kupasha habari.<br>• Amani: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi kwa utulivu. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Masuala ya usalama: mwanafunzi anaposhiriki katika kupasha habari kuhusu suala la ulanguzi wa binadamu.<br>• Ulanguzi wa binadamu: mwanafunzi anapowapasha wenzake habari kuhusu ulanguzi wa binadamu. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uzungumzaji wa kupasha habari katika somo la Kiswahili na uzungumzaji huo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ulanguzi wa binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.2 Kusoma** | **8.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>**Novela**<br><br>• *Mandhari*<br>• *Ploti*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mandhari na ploti katika fasihi,<br>b) kutambua mandhari mbalimbali na ploti ya novela,<br>c) kueleza umuhimu wa mandhari na ploti ya novela,<br>d) kuandika maelezo mafupi kuhusu mandhari na ploti ya novela aliyosoma,<br>e) kuchangamkia nafasi ya mandhari na ploti katika kazi ya fasihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya mandhari katika fasihi,<br>• kutambua mandhari mbalimbali katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kujadili umuhimu wa mandhari ya novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu mandhari,<br>• kuandika maelezo mafupi kuhusu mandhari ya novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kueleza maana ya ploti katika fasihi,<br>• kutambua ploti ya novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kujadili umuhimu wa ploti ya novela iliyoteuliwa na | 1. Ni mandhari gani unayokumbuka yaliyo katika kazi za fasihi ulizowahi kusoma?<br>2. Ploti ya hadithi ina vipengele gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mwalimu akishirikiana na wenzake,<br>• kuandika maelezo mafupi kuhusu ploti ya novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kuwawasilishia wenzake darasani uchambuzi wake kuhusu ploti,<br>• kumsomea mzazi au mlezi novela iliyochapishwa au kutoka mtandaoni na kutambua mandhari na ploti yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotambua na kujadili mandhari na ploti katika novela akiwa na wenzake katika kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha kazi yake darasani.
- Ubunifu: mwanafunzi anapochanganua habari katika novela ili kupata mandhari na ploti.
- Uwazaji kina: mwanafunzi anapoeleza umuhimu wa mandhari na ploti katika novela.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotafiti na kujiandaa ili awawasilishie wenzake muhtasari wa mandhari na ploti.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapotambua na kujadili mandhari na ploti kwenye novela katika kikundi.

| |
|---|
| • Upendo: mwanafunzi anapotoa maoni kuhusu uwasilishaji wa wengine ili kuwarekebisha na kuwahimiza.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anaposoma na kuchanganua novela.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wengine katika kikundi ili kutambua na kujadili mandhari na ploti kwenye novela. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuala mtambuko anuwai kulingana na maudhui yaliyoangaziwa katika novela. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mandhari na ploti katika shairi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ulanguzi wa binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.3 Kuandika** | **8.3.1 Viakifishi**<br>• *Kiulizi*<br>• *Koma*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua matumizi ya kiulizi na koma katika matini,<br>b) kutumia kiulizi na koma ipasavyo katika matini,<br>c) kufurahia matumizi bora ya kiulizi na koma katika matini. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua matumizi ya kiulizi (*k.v. mwishoni mwa sentensi ya swali)* na koma (*k.v. kutenga orodha ya vitu vitatu au kuandika anwani)* katika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kwenye matini andishi au za kidijitali,<br>• kutumia kifaa cha kidijitali kusoma matumizi ya kiulizi na koma,<br>• kuandika maneno, sentensi au vifungu vya maneno kuhusu suala lengwa kwa kutumia kiulizi na koma ipasavyo,<br>• kuandika kwenye kifaa cha kidijitali kifungu kifupi kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kiulizi na koma ipasavyo na kuwasambazia wenzake kwenye mtandao ili wakitolee maoni,<br>• kushirikiana na mzazi au mlezi kutafiti mtandaoni au katika | 1. Je, kiulizi hutumiwa vipi katika maandishi?<br>2. Je, koma hutumiwaje katika sentensi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vitabu vya ziada kuhusu matumizi ya kiulizi na koma katika maneno, sentensi au vifungu. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadili matumizi ya kiulizi na koma.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika vifungu vyenye matumizi yafaayo ya kiulizi na koma ubunifu wake unajengeka.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi kutafiti mtandaoni au katika vitabu vya ziada kuhusu matumizi ya kiulizi na koma.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Haki za watoto: mwanafunzi anapoandika sentensi kwa kutumia viakifishi wenzake.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha matumizi ya kiulizi na koma katika somo la Kiswahili na matumizi hayo katika English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ulanguzi wa binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **8.4 Sarufi** | **8.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br>• *Ngeli ya A-WA*<br>• *Ngeli ya U-I*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya A-WA na U-I katika sentensi,<br>b) kutambua nomino za ngeli ya A-WA na U-I katika matini,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya A-WA na U-I katika matini kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya A-WA na U-I katika matini. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya A-WA na U-I katika sentensi na mafungu ya maneno,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu vifupi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya A-WA na U-I,<br>• kuchopoa nomino za ngeli ya A-WA na U-I kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au katika tarakilishi,<br>• kutaja majina ya vitu katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya A-WA na U-I,<br>• kutenga nomino za ngeli ya A-WA na U-I katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari, | Ni vitu gani katika mazingira yako vilivyo na majina yanayopatikana katika ngeli ya A-WA na U-I? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuunda sentensi au vifungu vifupi vyenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya A-WA na U-I akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la ulaguzi wa binadamu,<br>• kutunga sentensi zenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya A-WA na U-I akitumia nomino za vitu vilivyo katika mazingira ya nyumbani, na kumsomea mzazi au mlezi wake ili amtolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kazi ya kikundi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi au vifungu akizingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya A-WA na U-I.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuunda sentensi au vifungu kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya A-WA na U-I.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizounda kwa kutumia nomino za ngeli ya A-WA na U-I katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.

| |
|---|
| • Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Haki na majukumu ya kibinadamu: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutenga nomino za ngeli ya A-WA na U-I katika sentensi na vifungu.<br>• Masuala ya usalama: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino za ngeli ya A-WA na U-I. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ngeli katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la ulanguzi wa binadamu na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

## 9.0 MATUMIZI YA VIFAA VYA KIDIJITALI KATIKA MAWASILIANO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **9.1.1 Kusikiliza kwa Kina**<br><br>*Sauti: /d/ na /nd/*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua sauti /**d**/ na /**nd**/ katika silabi na maneno,<br>b) kutamka sauti /**d**/ na /**nd/** ipasavyo ili kuzitofautisha kimatamshi katika silabi na maneno,<br>c) kuchangamkia matamshi bora ya sauti **/d/** na **/nd** /katika mazungumzo ya kawaida ili kufanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua sauti /**d**/ na /**nd**/ katika silabi na maneno (*k.v. doa/ndoa; duni/nduni; dugu/ndugu),*<br>• kutafuta maneno yenye sauti /**d**/ na /**nd**/ katika matini andishi na za kidijitali na kuyatamka ipasavyo,<br>• kusikiliza wenzake wakitamka maneno yenye sauti /**d**/ na /**nd**/ na kuwatolea maoni kwa heshima,<br>• kutunga vitanzandimi vinavyotumia sauti /**d**/ na /**nd**/ na kujirekodi kwa kutumia kifaa cha kidijitali,<br>• kusikiliza vitanzandimi alivyovirekodi ili kuvitathmini,<br>• kusikiliza vitanzandimi vinavyotumia sauti /**d**/ na /**nd**/ katika kifaa cha kidijitali, | Ni maneno yepi unayoyajua yaliyo na sauti /**d/** na /**nd/?** |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | • kuhakiki matamshi ya sauti /**d**/ na /**nd**/ kama zilivyotumiwa katika vitanzandimi alivyovisikiliza,<br>• kushiriki mazungumzo na mzazi au mlezi wake kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /**d/**na /**nd**/. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika mazungumzo na kutamka sauti /**d/** na /**nd/** ipasavyo.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza vitanzandimi vyenye sauti lengwa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotafuta maneno yenye sauti lengwa na kuyatamka ipasavyo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapotamka ipasavyo sauti lengwa na anapochangia katika kazi ya kikundi.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo na mzazi au mlezi kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti lengwa.

**Maadili:**

- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Usalama: mwanafunzi anapotamka na kutofautisha sauti lengwa na wenzake katika kikundi.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha matamshi ya sauti katika somo la Kiswahili na matamshi katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika mawasiliano na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-technical Studies.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.2 Kusoma** | **9.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Kushawishi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi,<br>b) kueleza maana ya msamiati na vifungu vya maneno katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi,<br>c) kueleza habari za kifungu cha ufahamu cha kushawishi kwa ufupi,<br>d) kuchangamkia usomaji wa ufahamu cha kushawishi ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe;<br>• kudondoa habari mahususi *(k.v. nani, nini, wapi na lini)* katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi,<br>• kueleza maana ya msamiati kuhusu suala lengwa (*k.v. maneno na nahau*) katika kifungu cha ufahamu cha kushawishi na kuueleza kwa kutumia kamusi,<br>• kuandika habari za kifungu cha ufahamu cha kushawishi kwa ufupi,<br>• kuwawasilishia wenzake kazi yake ili wamtolee maoni,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu cha ufahamu cha kushawishi na kujibu maswali. | Kifungu cha kushawishi kina sifa gani? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za kikundi.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kukamilisha kikamilifu kazi yake ya ufahamu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Usalama mtandaoni: mwanafunzi anaposoma kifungu cha ufahamu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha usomaji wa kifungu cha kushawishi katika somo la Kiswahili na katika somo la English
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika mawasiliano na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical Studies.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.3 Kuandika** | **9.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Masimulizi*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vinavyozingatiwa kujenga wazo katika insha ya masimulizi,<br>b) kueleza vipengele vinavyojenga wazo katika insha ya masimulizi,<br>c) kuandika insha ya masimulizi akikuza wazo katika aya ipasavyo,<br>d) kufurahia utunzi wa insha za masimulizi zenye mpangilio mzuri wa wazo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vipengele vinavyozingatiwa kujenga wazo (*k.v. mada, utangulizi, kati na hitimisho)* katika insha ya masimulizi kwenye matini za kimaandishi na za kidijitali,<br>• kueleza vipengele vinavyojenga mawazo,<br>• kuandika insha ya masimulizi akizingatia sehemu ya mwanzo, kati na hitimisho,<br>• kuwasomea wenzake insha aliyoandika au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni. | Ni sehemu gani kuu katika mpangilio wa matukio ya insha ya masimulizi? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika na kuwasomea wenzake insha aliyoiandika.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambazia insha.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya masimulizi yenye kuzingatia vipengele vifaavyo vya kujenga wazo.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuandika na kuwasomea wenzake insha. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Utunzi na haki za watoto: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi, anaposahihisha insha na wenzake na kujifunza ukakamavu, stahamala na kujiamini. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya masimulizi katika somo la Kiswahili na uandishi katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika mawasiliano na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-technical Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **9.4 Sarufi** | **9.4.1 Ngeli na Upatanisho wa Kisarufi**<br>• *Ngeli ya KI-VI*<br>• *Ngeli ya LI-YA*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI-VI na LI-YA katika sentensi,<br>b) kutambua nomino za ngeli ya KI-VI na LI-YA katika matini,<br>c) kutumia nomino za ngeli ya KI-VI na LI-YA katika matini kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino za ngeli ya KI-VI na LI-YA katika matini. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua viambishi vya upatanisho wa kisarufi vya ngeli ya KI-VI na LI-YA katika sentensi na mafungu vya maneno,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu vifupi kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi wa ngeli ya KI-VI na LI-YA,<br>• kuchopoa nomino za ngeli ya KI-VI na LI-YA kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno au tarakilishi,<br>• kutaja majina ya vitu katika mazingira ya shuleni yaliyo katika ngeli ya KI-VI na LI-YA,<br>• kutenga nomino za ngeli ya KI-VI na LI-YA katika orodha ya nomino, sentensi au vifungu kwenye vitabu, tarakilishi, chati | Utajuaje kama matini inazingatia kanuni za kisarufi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwa kuzikolezea wino au kuzipigia mstari,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi vyenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya KI-VI na LI-YA akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika mawasiliano,<br>• kuwasilisha kazi yake darasani au kuwasambazia wenzake mtandaoni ili waitolee maoni,<br>• kutunga sentensi zenye upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya KI-VI na LI-YA akitumia nomino za vitu vilivyo katika mazingira ya nyumbani, na kumsomea mzazi au mlezi wake ili amtolee maoni. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika kazi za kikundi.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi au vifungu vifupi akitumia nomino za ngeli ya KI-VI na LI-YA.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuunda sentensi au vifungu vifupi kwa kuzingatia upatanisho ufaao wa kisarufi wa ngeli ya KI-VI na LI-YA.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomsomea mzazi au mlezi wake sentensi alizounda kwa kutumia nomino za ngeli ya U-ZI na KI-VI na LI-YA katika mazingira ya nyumbani. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Mshkamano wa kijamiii: mwanafunzi anapochangia na kushirikiana na wenzake katika kikundi.<br>• Usalama mtandaoni: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia nomino katika ngeli ya KI-VI na LI-YA. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ngeli na upatanisho wa kisarufi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya vifaa vya kidijitali katika mawasiliano na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-technical Studies. |

# 10.0 KIJITHAMINI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **10.1.1 Nyimbo**<br>• *Nyimbo za Kazi*<br>• *Nyimbo za Dini*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya nyimbo za kazi na za dini ili kuzibainisha,<br>b) kutambua mazingira ambapo nyimbo za kazi na za dini huimbwa,<br>c) kueleza ujumbe katika nyimbo za kazi na za dini,<br>d) kuwasilisha nyimbo za kazi na za dini kwa kuzingatia hisia na ishara za mwili<br>e) kuchangamkia nyimbo za kazi na za dini kama vipera vya fasihi simulizi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kusikiliza kielelezo cha wimbo wa kazi na wa dini kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kifaa cha kidijitali,<br>• kueleza maana ya nyimbo za kazi na za dini ili kuzibainisha,<br>• kutambua mazingira ambapo nyimbo za kazi na za dini huimbwa akishirikiana na mwenzake,<br>• kueleza ujumbe katika nyimbo za kazi na za dini,<br>• kuwasilisha nyimbo za kazi na za dini kuzingatia hisia na ishara,<br>• kujirekodi akiimba nyimbo za kazi na za dini kwa kutumia vifaa vya kidijitali na kusikiliza akiwa na wenzake. | 1. Je, unajua nyimbo zipi katika jamii yako?<br>2. Je, nyimbo za kazi na za dini zinatofautianaje? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kutambua vipengele vya kimsingi vya nyimbo za kazi na dini kwenye kikundi.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza nyimbo mbalimbali za kazi na za dini. Pia anapojirekodi akiimba nyimbo za kazi na za dini.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapowasilisha nyimbo za kazi na za dini akizingatia hisia na ishara za mwili zifaazo.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapowasilisha nyimbo kwa wepesi na ukakamavu. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za uimbaji.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapochukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na pia kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Haki za watoto: mwanafunzi anapotunga na kuwasilisha nyimbo za kazi na za dini.<br>• Masuala mtambuko anuwai kulingana na maudhui yaliyoangaziwa katika nyimbo. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>Mwanafunzi anaweza kuhusisha uwasilishaji wa nyimbo katika somo la Kiswahili na uwasilishaji katika somo la English, na Creative Arts and Sports Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kujithamini na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llilopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.2 Kusoma** | **10.2.1 Kusoma kwa Kina** *Novela*<br><br>*Wahusika*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua wahusika katika novela,<br>b) kujadili sifa za wahusika katika novela,<br>c) kueleza uhusiano kati ya wahusika katika novela,<br>d) kuandika muhtasari wa sifa za wahusika katika novela,<br>e) kujadili mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika katika novela,<br>f) kujenga mazoea ya usomaji wa kazi za kifasihi katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua wahusika katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kujadili sifa za wahusika katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kuigiza wahusika katika novela iliyoteuliwa na mwalimu ili kukuza uelewa wa sifa zao,<br>• kueleza uhusiano kati ya wahusika katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kutazama video kuhusu wahusika katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>• kuandaa muhtasari kuhusu sifa za wahusika katika video aliyotazama,<br>• kujadili mafunzo yanayotokana na matendo ya wahusika,<br>• kumsimulia mzazi au mlezi wake hadithi ya novela na kujadiliana kuhusu wahusika wawili. | Ni mambo yapi yanayokuwezesha kuwaelewa wahusika katika novela? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Kujiamini: mwanafunzi anapoigiza na wenzake wahusika katika novela.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoigiza wahusika katika novela.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochambua sifa za wahusika katika novela.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika majadiliano ya kuwachambua wahusika katika kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Usalama: mwanafunzi anaposoma novela kutoka mtandaoni.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya wahusika katika novela katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kujithamini na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.3 Kuandika** | **10.3.1 Barua ya Kuomba Msamaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza umuhimu wa barua rasmi ya kuomba msamaha,<br>b) kutambua ujumbe katika barua rasmi ya kuomba msamaha,<br>c) kutambua vipengele vya kimuundo vya barua rasmi ya kuomba msamaha,<br>d) kuandika barua rasmi ya kuomba msamaha kwa kuzingatia ujumbe, muundo na lugha ifaayo,<br>e) kufurahia kujieleza kwa njia ifaayo kupitia kwa barua. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza umuhimu wa kuandika barua rasmi ya kuomba msamaha kuhusu matukio mbalimbali,<br>• kutambua ujumbe unaoafiki barua rasmi ya kuomba msamaha kwa kujadiliana na mwenzake,<br>• kujadili vipengele vya kimuundo vya barua rasmi ya kuomba msamaha,<br>• kujadili na wenzake kuhusu lugha inayofaa katika uandishi wa barua rasmi ya kuomba msamaha,<br>• kuandika barua rasmi ya kuomba msamaha kuhusu matukio mbalimbali na kuwasomea wenzake darasani ili waitolee maoni,<br>• kuandika barua ya kuomba msamaha katika kifaa cha kidijitali na kuwasambazia | Je, ni mambo gani yanayoweza kukufanya uandike barua rasmi ya kuomba msamaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake kupitia mtandao ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadili vipengele vya barua rasmi ya kuomba msamaha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika barua rasmi ya kuomba msamaha.
- Uwazaji kina: mwanafunzi anapowaza kuhusu matukio yanayomfanya mtu kuomba msamaha.
- Uraia: mwanafunzi anapoomba msamaha anajenga mshikamano katika jamii au taifa.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa nafasi wenzake kuchangia katika shughuli za ujifunzaji.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Masuala Mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapoandika barua ya kuomba msamaha.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa barua ya kuomba msamaha katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kujithamini na dhana ya msamaha katika somo la Kiswahili, na katika somo la Social Studies na Religious Education.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **10.4 Sarufi** | **10.4.1 Vinyume vya Maneno**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza dhana ya kinyume cha maneno,<br>b) kutambua vinyume vya nomino na vivumishi katika matini,<br>c) kutumia vinyume vya nomino na vivumishi katika matini,<br>d) kuchangamkia kutumia vinyume vya nomino na vivumishi katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya kinyume cha maneno,<br>• kutambua vinyume vya nomino na vivumishi kwa kutumia kadi maneno, mti maneno, kapu maneno,<br>• kutambua vinyume vya nomino na vivumishi katika orodha ya maneno, sentensi au vifungu,<br>• kuchagua sentensi zinazoashiria matumizi ya vinyume vya nomino na vivumishi kutoka kwa sentensi mbalimbali kwenye vitabu, tarakilishi au chati,<br>• kutumia vinyume vya nomino na vivumishi kujaza nafasi katika sentensi au vifungu,<br>• kutunga sentensi au kifungu kifupi kwa kutumia vinyume vya nomino na vivumishi ipasavyo akizingatia masuala | Je, dhana ya vinyume vya nomino ina maana gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mtambuko mbalimbali likiwemo suala la kijithamini,<br>• kusakura mtandaoni au katika vitabu vya ziada ili kupata vinyume zaidi vya nomino na vivumishi. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kazi ya kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua vinyume vya nomino na vivumishi.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha vinyume vya nomino na vivumishi.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposhiriki katika kutambua vinyume vya nomino na vivumishi na kuvitungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Kujithamini: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuchopoa vinyume vya nomino na vivumishi na kutunga sentensi sahihi.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya vinyume vya maneno katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la kujithamini na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

SNK Educational Consulting

## 11.0 MAJUKUMU YA WATOTO

| **Mada** | **Mada Ndogo** | **Matokeo Maalum Yanayotarajiwa** | **Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa** | **Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa** |
|---|---|---|---|---|
| **11.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **11.1.1 Kuzungumza kwa Kuambatanisha na Vitendo/Ishara**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara,<br>b) kutambua umuhimu wa kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara,<br>c) kujadili vitendo au ishara vya kuambatanisha na mazungumzo,<br>d) kutoa mazungumzo kwa kuyaambatanisha na | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana ya kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo,<br>• kutambua umuhimu wa kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara (*k.v. kumwelekeza mtu njia na kueleza jinsi ya kutayarisha chakula*),<br>• kuigiza jinsi ya kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo,<br>• kushiriki na wenzake katika kikundi kusikiliza au kutazama | 1. Ni vitendo gani tunatumia tunapozungumza?<br>2. Kuna umuhimu gani wa kutumia vitendo tunapozungumza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | vitendo au ishara zifaazo,<br>e) kujenga mazoea ya kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara ili kufanikisha mawasiliano. | mazungumzo yanayoambatanisha vitendo au ishara kutoka kwa mwalimu, mgeni mwalikwa au kwenye vifaa vya kidijitali,<br>• kujadili vitendo au ishara za kuambatanisha na mazungumzo,<br>• kusikiliza au kutazama mazungumzo yanayoambatana na vitendo au ishara kuhusu suala lengwa na kubainisha vipengele vya kuzungumza kwa aina hii vilivyozingatiwa,<br>• kuwasilisha mazungumzo yanayoambatana na | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | vitendo au ishara kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia vitendo au ishara zifaazo,<br>• kushiriki na mzazi au mlezi wake katika kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara kuhusu suala lengwa. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotumia lugha nyepesi kuwaelimisha wenzake kuhusu majukumu ya watoto huku akiambatanisha na vitendo au ishara.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposhiriki katika kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo na kufafanua namna ya kutekeleza jambo fulani.
- Ubunifu: mwanafunzi anapowasilisha mazungumzo kuhusu suala lengwa kwa kutumia mbinu zifaazo za kufanikisha mazungumzo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapojadili na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kuzungumza na kuambatanisha na vitendo katika kikundi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake zamu ya kushiriki katika mazungumzo bila kuwakata kauli.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapovitunza vifaa vya kidijitali anavyovitumia kuwaelezea wenzake kuhusu suala fulani.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki na wengine na kuchangia katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhiriki mazungumzo kwa kuambatanisha na vitendo kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara katika somo la Kiswahili na somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.2 Kusoma** | **11.2.1 Kusoma kwa Mapana**<br><br>*Matini ya kujichagulia*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza ujumbe wa matini ya kujichagulia,<br>b) kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia,<br>c) kutumia ipasavyo msamiati aliosoma katika matini ya kujichagulia,<br>d) kutoa muhtasari wa matini ya kujichagulia aliyosoma,<br>e) kujenga mazoea ya kusoma matini mbalimbali katika maisha ya kila siku. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza ujumbe wa matini ya kujichagulia aliyosoma,<br>● kutambua msamiati uliotumiwa katika matini ya kujichagulia (*andishi au ya kidijitali*,<br>● kutumia kamusi kutafuta maana za maneno asiyoyajua,<br>● kujenga rekodi ya msamiati aliojifunza katika kitabu,<br>● kumtunga sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma na kuwasomea wenzake darasani,<br>● kutoa muhtasari wa matini ya kujichagulia aliyosoma na kuwasilisha kwa wenzake ili waitolee maoni,<br>● kusakura mtandaoni na kujichagulia matini ya ziada kisha aisome. | 1. Unapenda kusoma matini za aina gani?<br>2. Unazingatia nini unapochagua matini ya kujisomea? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotangamana na wenzake na kuwawasilishia muhtasari wa matini ya kujichagulia aliyosoma.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi kutokana na msamiati wa matini ya kujichagulia akizingatia ufasaha wa lugha.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapomtungia mwenzake sentensi akitumia msamiati katika matini aliyoisoma.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapojichagulia matini ya kusoma na kutafuta maana za maneno asiyoyajua kwenye kamusi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anaposakura mtandaoni na kujichagulia matini ya kusoma. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake wanapowasilisha muhtasari wa matini ya kujichagulia waliyosoma.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kutafuta na kusoma matini aliyojichagulia. Pia anapozingatia nidhamu anaposakura mtandaoni.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutunga sentensi akitumia msamiati aliojifunza. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Masuaia ya kijinsi: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa mapana katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.3 Kuandika** | **11.3.1 Insha za Kubuni**<br><br>*Maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya mpangilio wa insha ya maelezo,<br>b) kueleza mpangilio wa insha ya maelezo,<br>c) kuandika insha ya maelezo inayozingatia mpangilio ufaao wa maelezo,<br>d) kufurahia kuandika ins ha za maelezo katika maisha ya kila siku akizingatia mpangilio ufaao wa maelezo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua mpangilio wa insha ya maelezo katika matini za kimaandishi au za kidijitali *(k.v. mpangilio unaozingatia mahali, hasa kama maelezo yanahusu mahali na mpangilio unaozingatia mfuatano wa matukio kiwakati)*,<br>● kueleza jinsi maelezo yalivyopangwa katika kielelezo cha insha ya maelezo,<br>● kuandika vidokezo vya insha vinavyozingatia jinsi maelezo yalivyopangwa katika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa,<br>● kuandika insha ya maelezo akizingatia mpangilio ufaao wa maelezo,<br>● kuwasomea wenzake insha aliyoiandika au awasambazie | Je, unawezaje kupanga matukio katika insha ya maelezo vipi? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapoandika insha na kuwasomea wenzake darasani.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuwasambazia wenzake insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha yenye mpangilio mzuri wa maelezo.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake kwa ufasaha insha aliyoandika ili waikosoe pamoja.
- Kujiamini: mwanafunzi anapoandika insha na kuwasomea wenzake.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
- Mshikamano wa kijamiii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na pia anaposahihisha insha na wenzake.
- Majukumu ya watoto: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **11.4 Sarufi** | **11.4.1 Mnyambuliko wa Vitenzi**<br>*Kauli ya:*<br>• *Kutenda*<br>• *Kutendea*<br>• *Kutendwa*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa katika vitenzi,<br>b) kutumia vitenzi katika kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa ipasavyo,<br>c) kuchangamkia kutumia ipasavyo vitenzi katika kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa ili kujenga ufasaha wa lugha. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua vitenzi katika kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa,<br>• kuteua vitenzi katika kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa, kwenye chati, kadi maneno, kapu maneno, sentensi na vifungu au tarakilishi,<br>• kujaza nafasi katika sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa ipasavyo,<br>• kugeuza vitenzi katika kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa,<br>• kutunga sentensi au vifungu vifupi kwa kutumia vitenzi katika kauli ya kutenda, kutendea na kutendwa akizingatia masuala mbalimbali likiwemo suala la majukumu ya watoto. | Ni kauli gani za vitenzi unazozijua? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika shughuli za ujifunzaji.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kutambua vitenzi katika kauli mbalimbali.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia vitenzi katika kauli mbalimbali.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapotambua viambishi vya kauli mbalimbali. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kuteua vitenzi katika kauli mbalimbali.<br>● Majukumu ya watoto: mwanafunzi anapoandika kifungu kuhusu suala lengwa kwa kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya mnyambuliko wa vitenzi katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la majukumu ya watoto na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

## 12.0 MAGONJWA AMBUKIZI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **12.1.1 Kusikiliza kwa Makini**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua hoja muhimu katika habari aliyosikiliza,<br>b) kuwasilisha hoja muhi mu katika habari,<br>c) kujenga mazoea ya kutambua hoja katika habari anayosikiliza ili kuimarisha usikilizaji wa makini. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua hoja muhimu katika habari aliyosikiliza kuhusu suala lengwa,<br>● kusikiliza habari kuhusu suala lengwa na kutaja hoja muhimu kwa maneno machache,<br>● kutafiti mtandaoni kuhusu suala lengwa na kuwawasilishia wenzake hoja muhimu kuhusu suala hilo kwa maneno machache,<br>● kumsomea mzazi au mlezi habari kuhusu suala lengwa na kushirikiana kutambua hoja. | Kwa nini ni muhimu kutambua hoja katika habari uliyosikiliza? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowatolea wenzake hoja muhimu katika habari aliyosikiliza inayochangia uelewa wa suala hilo.<br>● Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anaposikiliza habari, kuichanganua na kutambua hoja muhimu.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoiwasilisha upya habari aliyosikiliza kupitia hoja kuu. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapowapa wengine fursa ya kutambua na kusema hoja muhimu bila kuwakatiza.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia kujifunzia. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Magonjwa ya kuambukizwa na yasiyoambukizwa: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika mazungumzo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine**:<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza kwa makini katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa ambukizi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.2 Kusoma** | **12.2.1 Kusoma kwa Ufasaha**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kusoma kifungu kwa kuzingatia matamshi bora,<br>b) kusoma kifungu kwa kasi ifaayo,<br>c) kusoma kifungu kwa kutumia sauti ipasavyo,<br>d) kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo,<br>e) kuridhia kusoma makala kwa kuzingatia vipengele vinavyofanikisha mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kujadiliana na wenzake vipengele vya kuzingatia katika kusoma makala kwa ufasaha,<br>● kutazama vielelezo vya video za watu wanaosoma makala kwa ufasaha makala *(k.v. hotuba na habari),*<br>● kusoma kifungu kuhusu suala lengwa katika matini andishi au ya kidijitali akizingatia matamshi bora,<br>● kusoma kifungu kuhusu suala lengwa kwa kuzingatia kasi ifaayo (*maneno sahihi yasiyopungua 95 kwa dakika*),<br>● kusoma kifungu akizingatia sauti ifaayo *(k.v. kiwango cha sauti na kiimbo),*<br>● kusoma kifungu kwa kuambatanisha ishara zifaazo | Unazingatia nini ili kusoma makala kwa ufasaha? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | panapofaa *(k.v. ishara za uso na mikono),*<br>● kusoma mbele ya wenzake kazi yake ili wamtolee maoni,<br>● kumsomea mzazi au mlezi makala akizingatia vipengele vya usomaji bora. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapofanikiwa kusoma makala kwa ufasaha na anapojadiliana na wenzake katika kikundi kuhusu vipengele vya kimsingi vya kusoma kwa ufasaha.
- Kujiamini: mwanafunzi anaposoma kifungu kwa ufasaha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotumia ishara wakati wa kusoma kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli ya kusoma anakuza hamu ya ujifunzaji.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi wanapojadili vipengele vya usomaji bora.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika mjadala wakati wa shughuli ya ujifunzaji katika kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi kujadili vipengele vya usomaji bora.

**Masuala Mtambuko:**

Magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa: mwanafunzi anaposoma kifungu kuhusu magonjwa ambukizi.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha kusoma kwa ufasaha katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa ambukizi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.3 Kuandika** | **12.3.1 Hotuba ya Kupasha Habari**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya hotuba ya kupasha habari,<br>b) kutambua hotuba ya kupasha habari katika matini,<br>c) kueleza ujumbe, lugha na muundo wa hotuba ya kupasha habari,<br>d) kuandika hotuba ya kupasha habari kwa kuzingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao,<br>e) kuchangamkia nafasi ya hotuba ya kupasha habari katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya hotuba ya kupasha habari,<br>● kujadiliana na wenzake kuhusu ujumbe, lugha na muundo ufaao wa hotuba ya kupasha habari,<br>● kujadili na wenzake miktadha inayochochea hotuba ya kupasha habari,<br>● kujadili na wenzake vidokezo vinavyoweza kutumiwa katika kuandika hotuba ya kupasha habari,<br>● kuandika hotuba ya kupasha habari kuhusu suala lengwa akizingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao kisha awasambazie wenzake mtandaoni au kuwasomea darasani ili waitolee maoni,<br>● kuandika hotuba ya kupasha habari kuhusu suala linaloathiri | Ni mambo yepi ambayo yanaweza kuelezwa kupitia kwa hotuba? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | jamii yao na kumsomea mzazi au mlezi wake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotoa mchango wake katika kikundi kuhusu hotuba ya kupasha habari.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika hotuba ya kupasha habari na kuisambaza kwa mtandao.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoandika hotuba ya kupasha habari.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoandika ya kupasha habari kuhusu suala linaloathiri jamii yao na kumsomea mzazi au mlezi wake.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe, lugha na muundo wa hotuba ya kupasha habari.
- Elimu ya afya na kujikinga: mwanafunzi anapoandika hotuba ya kupasha habari kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa hotuba ya kupasha Habari katika somo la Kiswahili na uandishi huo katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa ambukizi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **12.4 Sarufi** | **12.4.1 Aina za Sentensi**<br>• *Sentensi Sahili*<br>• *sentensi ambatano*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya sentensi sahili na ambatano,<br>b) kutambua sentensi sahili na ambatano katika matini,<br>c) kutunga sentensi sahili na ambatano ipasavyo,<br>d) kuchangamkia matumizi ya sentensi sahili na ambatano katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya sentensi sahili na ambatano,<br>● kutenga sentensi sahili na ambatano katika orodha ya sentensi kwenye vitabu, chati au tarakilishi kwa kuzipigia mstari au kuzikolezea wino,<br>● kutaja sentensi sahili na ambatano zinazojitokeza katika vifungu,<br>● kuunganisha sentensi sahili mbili au zaidi kuunda sentensi ambatano<br>● kuunda sentensi sahili kutokana na sentensi ambatano<br>● kutunga sentensi sahili na ambatano ipasavyo akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la magonjwa ambukizi,<br>● kumtungia mzazi au mlezi sentensi sahili na ambatano zinazohusu | 1. Ni aina gani ya sentensi unazozijua?<br>2. Je, sentensi sahili na ambatano hutofautianaje? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | shughuli katika mazingira ya nyumbani. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotaja sentensi sahili na ambatano zinazojitokeza katika vifungu akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua sentensi sahili na ambatano.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia sentensi sahili na ambatano.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua sentensi sahili na ambatano katika kifungu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtungia mzazi au mlezi wake sentensi sahili na ambatano zinazohusu shughuli katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutunga sentensi sahili na ambatano.
- Magonjwa yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa: mwanafunzi anapotunga sentensi sahili na ambatano kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha aina za sentensi katika somo la Kiswahili na katika somo la English.

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la magonjwa ambukizi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Integrated Science na Agriculture.

## 13.0 UTATUZI WA MIZOZO

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **13.1.1 Wahusika katika Nyimbo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua wahusika katika wimbo,<br>b) kuchambua wahusika katika wimbo,<br>c) kueleza mafunzo kutokana na wahusika katika wimbo,<br>d) kufurahia kushiriki katika uchanganuzi wa wahusika katika nyimbo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kusikiliza wimbo na kutambua<br>● wahusika katika wimbo huo *(k.v. mwimbaji, hadhira lengwa na wahusika wengine kwenye wimbo),*<br>● kuchambua wahusika katika wimbo aliousikiliza,<br>● kusikiliza na kuimba wimbo katika vifaa vya kidijitali kuhusu suala lengwa akiwa na wenzake huku akichukua nafasi mbalimbali *(k.v. mwimbaji au hadhira),*<br>● kusikiliza wimbo katika vifaa vya kidijitali na kueleza mafunzo kutokana na wahusika katika wimbo huo, | Je, wahusika katika wimbo? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kutunga wimbo kuhusu mada lengwa na kuwawasilishia wenzake ili kuchanganua wahusika,<br>● kushirikiana na mzazi au mlezi kuchanganua wahusika katika nyimbo mbalimbali kutoka kwa jamii yake. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi na kuchambua wahusika kwa njia wazi akiwa na wenzake.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia nyimbo.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga wimbo kuhusu suala lengwa na kuwawasilishia wenzake.
- Uwazaji kina na utatuzi wa matatizo: mwanafunzi anapochanganua wahusika na nafasi zao katika wimbo.
- Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake wimbo alioutunga.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi na kutunza vifaa vya kidijitali anavyotumia.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Utatuzi wa mizozo: mwanafunzi anapoimba nyimbo kuhusu suala lengwa.<br>● Masuala ya kijamii: mwanafunzi anapoimba nyimbo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya wahusika katika nyimbo katika somo la Kiswahili na English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utatuzi wa mizozo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.2 Kusoma** | **13.2.1 Kusoma kwa Kina**<br><br>*Mbinu za Lugha*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya mbinu za lugha katika fasihi,<br>b) kutambua mbinu za lugha katika novela,<br>c) kueleza umuhimu wa mbinu za lugha zilizotumiwa katika novela,<br>d) kufurahia kuchanganua matumizi ya mbinu za lugha katika fasihi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya mbinu za lugha katika fasihi,<br>● kutambua mbinu za lugha *(k.v. tashbihi, sitiari, nahau, methali, tasfida na tanakali za sauti)* katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kueleza umuhimu wa mbinu za lugha zilizotumiwa katika novela iliyoteuliwa na mwalimu,<br>● kuhakiki uwasilishaji wa wenzake na kutoa maoni,<br>● kufanya utafiti maktabani au mtandaoni kuhusu matumizi ya mbinu za lugha katika novela,<br>● kumtajia mzazi au mlezi matumizi ya mbinu za lugha katika novela aliyosoma. | Mbinu za lugha zina umuhimu gani zinapotumiwa katika kifungu? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kutambua mbinu za lugha kwenye novela aliyosoma akiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapowawasilishia wenzake muhtasari wa matumizi ya mbinu za lugha katika novela kwa kutetea hoja zake.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapofanya utafiti maktabani na mtandaoni kuhusu matumizi ya mbinu za lugha katika novela. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapotangamana na wenzake katika kikundi kujadili mbinu za lugha katika novela huku akiheshimu maoni yao.<br>● Upendo: mwanafunzi anapohakiki uwasilishaji wa wenzake huku akiwakosoa kwa upendo na kuwahimiza.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojiandaa ipasavyo ili kuwawasilishia wenzake kazi yake. Pia anapochukua hatua ya kutafiti kuhusu matumizi ya mbinu za lugha maktabani au mtandaoni.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Utatuzi wa mizozo: mwanafunzi anapoeleza ujumbe katika Novela. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha mbinu za lugha katika novela ya Kiswahili na ya English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utatuzi wa mizozo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.3 Kuandika** | **13.3.1 Insha ya Kubuni**<br><br>*Maelezo*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua mambo ya kimsingi katika uandishi wa insha ya maelezo,<br>b) kuandika insha ya maelezo inayodhihirisha sifa za mtu,<br>c) kuchangamkia kutoa maelezo kamilifu kuhusu kitu au jambo. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua mambo ya kimsingi katika uandishi wa insha ya maelezo,<br>• kuandaa vidokezo vya insha ya maelezo kuhusu sura na matendo ya mtu anayelengwa katika insha hiyo,<br>• kuandika daftarini au katika kifaa cha kidijitali insha ya maelezo inayotoa sifa za mtu akizingatia muundo ufaao na inayohusisha suala lengwa kisha awasomee wenzake darasani au awasambazie wenzake mtandaoni ili waitolee maoni,<br>• kutolea insha za wenzake maoni kwa upendo. | 1. Je, insha ya maelezo inahusu nini?<br>2. Je, ni vigezo vipi vinatumika katika kuandika insha ya maelezo? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadiliana kuhusu insha ya maelezo.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kuandika insha ya maelezo na kuisambaza mtandaoni.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapoandika insha ya maelezo kwa muundo ufaao.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapobuni na kusambaza insha kwa wenzake. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.<br>● Upendo: mwanafunzi anapotolea insha za wenzake maoni. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Utatuzi wa mizozo: mwanafunzi anapoandika insha kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha ya maelezo katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utatuzi wa mizozo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **13.4 Sarufi** | **13.4.1 Ukanushaji kwa Kuzingatia Nyakati**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana ya ukanushaji,<br>b) kutambua wakati uliopita, uliopo na ujao katika matini,<br>c) kutambua ukanushaji kwa kuzingatia wakati uliopita, uliopo na ujao katika matini,<br>d) kutumia ipasavyo hali ya ukanushaji wa wakati uliopita, uliopo na ujao katika matini,<br>e) kuchangamkia kukanusha sentensi katika wakati uliopita, uliopo na ujao ili kukuza mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kueleza maana ya ukanushaji,<br>● kutambua nyakati tatu tofauti *(uliopita, uliopo, ujao)* kutoka kwenye chati, mti maneno, vitabu au vifaa vya kidijitali,<br>● kutambua ukanushaji wa sentensi katika wakati uliopita, uliopo na ujao,<br>● kukanusha sentensi alizopewa katika wakati uliopita, uliopo na ujao,<br>● kutunga sentensi au vifumgu vifupi kwa kutumia wakati uliopita, uliopo na ujao na kuzikanusha akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la utatuzi wa mizozo,<br>● kuwasilisha kazi yake darasani au kuwasambazia | Tunakanusha sentensi kwa kuzingatia nyakati gani? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wenzake mtandaoni ili kuitolea maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki kikamilifu katika kazi za kikundi.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua ukanushaji kwa kuzingatia nyakati.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuonyesha ukanushaji wa nyakati.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kutambua ukanushaji wa nyakati na kuutungia sentensi sahihi.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anapotunga sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ukanushaji katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la utatuzi wa mizozo na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies.

## 14.0 MATUMIZI YA PESA

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **14.1.1 Lugha katika Nyimbo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua vipengele vya lugha vinavyotumika katika nyimbo,<br>b) kujadili umuhimu wa vipengele vya lugha vinavyotumika katika nyimbo teule,<br>c) kuonea fahari uchanganuzi wa lugha katika nyimbo kama utungo wa fasihi simulizi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua vipengele vya lugha kwa kusikiliza nyimbo kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu, kwenye maandishi *(k.v. vitabu na chati)* au vifaa vya kidijitali,<br>● kujadili umuhimu wa vipengele vya lugha vilivyotumika katika nyimbo alizozisikiliza,<br>● kutunga wimbo unaohusiana na suala lengwa akizingatia vipengele vya lugha katika nyimbo,<br>● kushirikiana na mzazi au mlezi wake kusikiliza nyimbo katika jamii yake na kutambua vipengele vya lugha katika nyimbo. | 1. Nyimbo hutumia vipengele gani vya lugha?<br>2. Kutumia vipengele mbalimbali vya lugha katika wimbo kuna umuhimu gani? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>● Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapotambua vipengele vya lugha katika nyimbo wakiwa na wenzake katika kikundi.<br>● Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kusikiliza nyimbo.<br>● Ubunifu: mwanafunzi anapotunga wimbo na kuzingatia vipengele vya lugha.<br>● Kujiamini: mwanafunzi anapojadili na wenzake katika kikundi vipengele vya lugha katika nyimbo kwa njia wazi.<br>● Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhirikiana na mzazi au mlezi wake kusikiliza nyimbo na kutambua vipengele vya lugha vilivyotumika. |
| **Maadili:**<br>● Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>● Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>● Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotunga nyimbo kuhusu suala lengwa.<br>● Uwekaji wa malengo ya kifedha: mwanafunzi anaposikiliza nyimbo kutoka kwa mwalimu na kutunga nyimbo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya nyimbo katika somo la Kiswahili na dhana hiyo katika somo la English na Creative Arts and Sports<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya pesa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical, Mathematics na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.2 Kusoma** | **14.2.1 Kusoma kwa Ufahamu**<br><br>*Kifungu cha Mjadala*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kudondoa habari mahususi katika kifungu cha mjadala,<br>b) kutambua msamiati mpya katika kifungu cha mjadala,<br>c) kuandika habari za kifungu cha mjadala kwa ufupi,<br>d) kuchambua mitazamo katika kifungu cha mjadala,<br>e) kuridhia kusoma kwa ufahamu ili kukuza uelewa wa habari. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kudondoa habari mahususi *(k.v. nani, nini, wapi, lini)* katika kifungu cha mjadala cha ufahamu,<br>● kutambua msamiati kuhusu suala lengwa katika kifungu cha mjadala na kuueleza kimuktadha au kwa kutumia kamusi,<br>● kuandika habari za kifungu cha ufahamu kwa ufupi,<br>● kuchambua mitazamo iliyo katika kifungu cha ufahamu cha mjadala,<br>● kuwawasilishia wenzake kazi yake ili wamtolee maoni,<br>● kutathmini kazi ya wenzake kwa upendo, | 1. Kwa nini tunasoma ufahamu?<br>2. Je, ni mambo gani yanayoweza kukusaidia kuelewa kifungu cha ufahamu? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | ● kumsomea mzazi au mlezi kifungu cha ufahamu na kujibu maswali. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**
- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapowasilisha kazi yake ya ufahamu kwa wenzake.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kukamilisha kikamilifu kazi yake ya ufahamu.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za ujifunzaji.

**Maadili:**
- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapotathmini kazi ya wenzake kwa upendo.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**
Matumizi ya pesa: mwanafunzi anaposoma kifungu cha ufahamu kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha usomaji wa kifungu cha mjadala katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya pesa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical, Mathematics na Religious Education.

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.3 Kuandika** | **14.3.1 Insha ya Maelekezo**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua aina za insha za maelekezo,<br>b) kujadili sifa za insha ya maelekezo,<br>c) kuandaa mpangilio wa hatua za insha ya maelekezo,<br>d) kuandika insha ya maelekezo akizingatia vipengele muhimu vya insha ya maelekezo,<br>e) kufurahia kutoa maelekezo ifaavyo katika maisha ya kila siku akizingatia anwani na mpangilio ufaao wa hatua. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kubainisha sifa za insha ya maelekezo kwa kuzingatia vielelezo vya insha kwenye matini za kimaandishi au za kidijitali (*k.v. usahihi wa habari, mpangilio wa maelezo wenye mantiki, lugha sahili na maelezo yanayotoka upande mmoja*),<br>● kujadili na wenzake aina za insha za maelekezo,<br>● kushiriki katika kikundi kujadili mpangilio ufaao wa hatua za kuelekeza,<br>● kuandaa mpangilio wa hatua za insha ya maelekezo,<br>● kuandika insha ya maelekezo akizingatia anwani na mpangilio mwafaka wa hatua huku akitumia vipengele vya | Utatumia mpangilio gani wa kumwelekeza mtu asipoteze njia? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | lugha vinavyotumiwa kuelekeza ili kumjengea msomaji taswira kamili ya anachoelekezwa kufanya,<br>● kuwasomea wenzake katika kikundi insha aliyoandika darasani au awasambazie kwenye vifaa vya kidijitali ili waitolee maoni. | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na wenzake katika kujadili kuhusu anwani na hatua katika kielelezo cha insha ya maelekezo waliyosoma.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusambaza insha.
- Ubunifu: mwanafunzi anapoteua lugha mwafaka na kufaulu kutoa maelezo bayana ya anachoelekeza.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapowasomea wenzake insha aliyoandika ili waitolee maoni.
- Kujiamini: mwanafunzi anapofaulu kuwasomea wenzake insha hadharani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

| |
|---|
| **Masuala Mtambuko:**<br>● Elimu ya kifedha: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kusahihisha insha ya maelezo na wenzake na kujifunza ukakamavu, stahamala na kujiamini.<br>● Ukadiriaji wa matumizi ya pesa-mwanafunzi anapoandika insha ya maelekezo kuhusu suala kuu. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa insha za maelekezo katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>● Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya pesa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical, Mathematics na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **14.4 Sarufi** | **14.4.1 Ukubwa wa Nomino**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua nomino katika hali ya ukubwa katika matini,<br>b) kutambua viambishi vya ukubwa katika nomino,<br>c) kutumia nomino katika hali ya ukubwa ipasavyo,<br>d) kuchangamkia kutumia nomino katika hali ya ukubwa katika sentensi. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>● kutambua nomino katika hali ya ukubwa (*k.v. jitu, joka, jiji, kapu, goma, jisu na jishamba)* kwenye orodha ya nomino, chati, kadi maneno, kapu maneno, sentensi, vifungu vya maneno au tarakilishi,<br>● kutambua viambishi vya ukubwa katika maneno,<br>● kuandika majina ya vifaa vya darasani katika ukubwa,<br>● kuambatanisha nomino za hali ya wastani na za hali ya ukubwa kwa usahihi,<br>● kubadilisha nomino za hali ya wastani ziwe katika katika hali ya ukubwa,<br>● kujaza nafasi katika sentensi au vifungu kwa kutumia nomino katika hali ya ukubwa ipasavyo,<br>● kutunga sentensi au vifungu vifupi akitumia nomino katika hali ya ukubwa akizingatia masuala mtambuko | Unazingatia nini unapoandika nomino katika ukubwa? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | mbalimbali likiwemo suala la matumizi ya pesa,<br>● kuwasilisha kazi yake darasani ili wenzake waitathmini,<br>● kumtajia mzazi au mlezi majina ya vifaa vya nyumbani katika ukubwa (*k.v. jimeza, jijiko na jisahani*). | |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki na kuchangia katika kazi za kikundi kikamilifu.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali katika kutambua nomino katika hali ya ukubwa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahihi kuhusu suala lengwa akitumia nomino katika hali ya ukubwa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapomtajia mzazi au mlezi wake nomino katika hali ya ukubwa katika mazingira ya nyumbani.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Upendo: mwanafunzi anapowapa wenzake nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi anajifunza ukakamavu, stahamala na kujiamini.
- Elimu ya kifedha: mwanafunzi anapotunga sentensi mbalimbali kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ukubwa na udogo katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la matumizi ya pesa na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Pre-Technical, Mathematics na Religious Education.

## 15.0 MAADILI YA MTU BINAFSI

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Llililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.1 Kusikiliza na Kuzungumza** | **15.1.1 Kusikiliza Habari na Kujibu**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua masuala katika matini aliyosikiliza,<br>b) kutambua msamiati wa suala lengwa katika matini aliyosikiliza,<br>c) kutabiri yatakayotokea katika matini kutokana na vidokezo alivyosikia katika habari,<br>d) kueleza maana za msamiati wa suala lengwa kama ulivyotumiwa katika matini aliyosikiliza,<br>e) kuchangamkia kushiriki katika kusikiliza kwa | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua masuala yanayoshughulikiwa katika matini kuhusu suala lengwa,<br>• kutambua msamiati wa suala lengwa uliotumiwa katika matini alizosikiliza kutoka kwenye kifaa cha kidijitali, mwalimu au mgeni mwalikwa,<br>• kutabiri kitakachotokea au atakachofanya mhusika kutoka kwenye matini aliyosikiliza kwa kuzingatia vidokezo (*k.v. anwani na picha)* anavyopatana navyo katika usikilizaji, | Je, ni mambo gani yanayokuelekeza kufasiri suala muhimu katika habari unayosikiliza? |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | ufahamu ili kukuza stadi ya kusikiliza. | • kueleza maana za msamiati wa suala lengwa kama ulivyotumiwa katika matini aliyosikiliza,<br>• kusikiliza matini kuhusu suala lengwa kutoka kwa mwalimu au mgeni mwalikwa na kufasiri wazo kuu katika habari hiyo,<br>• kusikiliza habari kwenye vifaa vya kidijitali (*k.v. kinasasauti)* kuhusu suala lengwa na kutaja masuala yanayoshughulikiwa,<br>• kushirikiana na mzazi au mlezi kutafiti kwenye tovuti salama kuhusu maadili ya mtu binafsi na kutambua suala kuu au masuala makuu katika matini. | |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kikundi na kuchangia kutambua na kueleza maana za msamiati wa suala lengwa katika matini aliyosikiliza.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusikilizia habari na kujibu kulingana na maagizo.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anaposikiliza matini ipasavyo na anapochangia katika shughuli za kikundi.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposhiriki shughuli ya kusikiliza kwa ufahamu na mzazi au mlezi wake na kujifunza maaarifa ya kuwasilisha habari kuhusu maadili ya mtu binafsi. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika shughuli za kikundi; pia anapoheshimu zamu ya wenzake katika mazungumzo.<br>• Upendo: mwanafunzi anapowasikiliza wasemaji kwa makini. Pia anapowapa wanafunzi wenzake zamu ya kuzungumza.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapotunza vifaa vya kidijitali anavyotumia katika mazungumzo.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Maadili ya mtu binafsi**:** mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kusikiliza na kujibu mazungumzo kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya kusikiliza Habari na kujibu katika somo la Kiswahili na katika somo la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya mtu binafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.2 Kusoma** | **15.2.1 Ufupisho**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza kwa usahihi ujumbe wa aya za matini kwa sentensi mojamoja,<br>b) kueleza kwa usahihi ujumbe wa aya zote za matini kwa aya moja,<br>c) kuandika ufupisho unaozingatia mtazamo wa matini ya kufupishwa,<br>d) kufurahia kufupisha ujumbe kwa usahihi katika miktadha mbalimbali. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza kwa usahihi ujumbe katika kila aya kwa kutumia sentensi mojamoja,<br>• kueleza kwa usahihi ujumbe wa aya zote za matini kwa aya moja,<br>• kujadili katika kikundi kuhusu jinsi ya kuandika ufupisho wa matini,<br>• kumsomea mzazi au mlezi kifungu na kuandika ufupisho kutoka mtandaoni au vitabuni na kutambua ujumbe wa aya za matini. | Ni mambo gani yanayokusaidia kuandika ufupisho? |
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anapojadiliana na wenzake kuhusu ufupisho wa matini.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia vifaa vya kidijitali kusoma kifungu.<br>• Kujiamini: mwanafunzi anapofanya ufupisho wa matini katika kikundi.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anaposoma kifungu kutoka mtandaoni na kukifupisha. | | | | |

| |
|---|
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Upendo: mwanafunzi anapopewa nafasi ya kushiriki katika shughuli za ujifunzaji darasani na katika kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>• Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kutambua na kufupisha kifungu.<br>• Maadili ya mtu binafsi**:** mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kusoma na kufupisha kifungu kuhusu suala lengwa. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya ufupisho katika somo la Kiswahili na lile la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya mtu binafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Swali Dadisi Lililopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.3 Kuandika** | **15.3.1 Kuandika Kidijitali**<br><br>*Baruapepe*<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kutambua ujumbe unaoafiki baruapepe kwa rafiki,<br>b) kutambua vipengele vya kimuundo vya baruapepe kwa rafiki,<br>c) kutumia lugha inayofaa katika uandishi wa baruapepe kwa rafiki,<br>d) kuandika baruapepe kwa rafiki kwa kuzingatia ujumbe, lugha na muundo ufaao,<br>e) kujenga mazoea ya kuwasiliana kwa kuandika baruapepe kwa rafiki. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kutambua ujumbe unaoafiki baruapepe kwa rafiki kwa kujadiliana na mwenzake,<br>• kujadili vipengele vya kimuundo vya baruapepe kwa rafiki,<br>• kushiriki katika kujadili na wenzake kuhusu lugha inayofaa katika uandishi wa baruapepe kwa rafiki,<br>• kuandika baruapepe kwa rafiki kwenye tarakilishi na kumsambazia mwenzake kupitia mtandao ili aitolee maoni,<br>• kumwandikia mwalimu wake baruapepe kwa rafiki ili aitathmini. | Je, utazingatia nini unapoandika barua pepe kwa rafiki yako? |

| |
|---|
| **Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**<br>• Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe, lugha na muundo wa baruapepe kwa rafiki.<br>• Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotumia tarakilishi kuandika baruapepe kwa rafiki na kuisambaza mtandaoni.<br>• Ubunifu: mwanafunzi anapoandika baruapepe kwa rafiki.<br>• Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapoandika baruapepe kwa rafiki kwenye tarakilishi na kumsambazia mwalimu. |
| **Maadili:**<br>• Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.<br>• Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.<br>• Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi. |
| **Masuala Mtambuko:**<br>Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kikundi kujadili ujumbe, lugha na muundo wa baruapepe kwa rafiki. |
| **Uhusiano na Masomo Mengine:**<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha uandishi wa baruapepe katika somo la Kiswahili na lile la English.<br>• Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya mtu binafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education. |

| Mada | Mada Ndogo | Matokeo Maalum Yanayotarajiwa | Shughuli za Ujifunzaji Zilizopendekezwa | Maswali Dadisi Yaliyopendekezwa |
|---|---|---|---|---|
| **15.4 Sarufi** | **15.4.1 Usemi Halisi na Usemi wa Taarifa**<br><br>(Vipindi 2) | Kufikia mwisho wa mada ndogo, mwanafunzi aweze:<br>a) kueleza maana za usemi halisi na usemi wa taarifa,<br>b) kutambua kanuni za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa,<br>c) kutumia usemi halisi na usemi wa taarifa ifaavyo,<br>d) kuchangamkia matumizi ya usemi halisi na usemi wa taarifa katika mawasiliano. | Mwanafunzi aelekezwe:<br>• kueleza maana za usemi halisi na usemi wa taarifa,<br>• kutambua kanuni za kimsingi za kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa,<br>• kubadilisha sentensi sahili kutoka usemi halisi hadi usemi wa taarifa na usemi wa taarifa hadi usemi halisi,<br>• kutunga sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa akizingatia akizingatia masuala mtambuko mbalimbali likiwemo suala la maadili ya mtu binafsi,<br>• kuwasomea wenzake ili wamtolee maoni,<br>• kushirikiana na wenzake kutunga na kutathmini sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa. | 1. Ni kwa usemi gani tunaweza kuwasilisha ujumbe?<br>2. Je, ni mambo gani unayozingatia wakati wa kubadilisha usemi halisi kuwa usemi wa taarifa? |

**Umilisi wa Kimsingi Unaokuzwa:**

- Mawasiliano na ushirikiano: mwanafunzi anaposhiriki katika kazi za kikundi na kujadili usemi halisi na wa taarifa.
- Ujuzi wa kidijitali: mwanafunzi anapotambua sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa kwenye matini ya kidijitali.
- Kujiamini: mwanafunzi anapomsomea mwenzake sentensi sahili alizotunga za usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Ubunifu: mwanafunzi anapotunga sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa.
- Hamu ya ujifunzaji: mwanafunzi anapotunga na kutathmini sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa na wenzake.

**Maadili:**

- Heshima: mwanafunzi anapoheshimu maoni ya wenzake katika kazi ya kikundi.
- Uwajibikaji: mwanafunzi anapojitolea kuchukua nafasi mbalimbali katika shughuli za kikundi.
- Umoja: mwanafunzi anaposhiriki katika shughuli za kikundi.

**Masuala Mtambuko:**

- Mshikamano wa kijamii: mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake katika kutambua sentensi sahili za usemi halisi na usemi wa taarifa anakuza ukakamavu, stahamala na kujiamini.
- Maadili ya mtu binafsi**:** mwanafunzi anaposhirikiana na wenzake kutumia usemi halisi na wa taarifa katika sentensi kuhusu suala lengwa.

**Uhusiano na Masomo Mengine:**

- Mwanafunzi anaweza kuhusisha dhana ya usemi halisi na usemi wa taarifa katika somo la Kiswahili na katika somo la English.
- Mwanafunzi anaweza kuhusisha suala la maadili ya mtu binafsi na yale amejifunza kuhusu suala hilo katika somo la Social Studies na Religious Education.

## MWONGOZO WA VIGEZO NA VIWANGO VYA KUTATHMINIA ULIOPENDEKEZWA

| MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutumia vipengele vya kuzingatia katika usikilizaji.** *kutumia lugha ya adabu, kutomkata kalima mzungumzaji, ubadilishanaji zamu ufaao, kujibu kwa kujikita katika kiini cha swali/ mazungumzo* | Anatumia vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mazungumzo kwa wepesi. | Anatumia vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mazungumzo. | Anatumia baadhi ya vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mazungumzo. | Anatumia baadhi ya vipengele vifaavyo katika kusikiliza na kujibu mazungumzo kwa kwa kusaidiwa. |
| **Kusikiliza kwa kina** (*Matamshi ya sauti mbalimbali:/***dh/** *na* **/th/,** /**d**/ na /**nd/.** | Anasikiliza na kutambua sauti lengwa na kuzitamka kwa ufasaha. | Anasikiliza na kutambua sauti lengwa na kuzitamka. | Anasikiliza na kutambua baadhi ya sauti lengwa na kuzitamka. | Anasikiliza na kutambua baadhi ya sauti lengwa na kuzitamka akiongozwa. |
| **Kuweza kusikiliza na kufasiri ujumbe** *(kutambua ujumbe, kuuhusisha ujumbe katika* | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya kila siku. | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya kila siku kwa kiasi. | Anasikiliza na kufasiri ujumbe na kuuhusisha na maisha ya kila siku kwa kiasi akielekezwa |

| MADA: KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| *matini na maisha ya kila siku)* | kila siku kwa utendeti. | | | |
| **Kuweza kuzungumza na kujieleza kwa ufasaha** *(uzungumzaji wa papo kwa papo, uzungumzaji wa kutumia vidokezo, kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo, maamkuzi na maagano,)* | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia aina mbalimbali za uzungumzaji kwa ubunifu. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia aina mbalimbali za uzungumzaji. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya aina za uzungumzaji. | Anazungumza na kujieleza kwa ufasaha akizingatia baadhi ya aina za uzungumzaji akielekezwa. |
| **Kuweza kuwasilisha utungo wa fasihi simulizi au andishi.** (F*asihi andishi na simulizi, nyimbo za watoto na bembelezi, nyimbo za kazi na za dini. Wahusikaa katika nyimbo, lugha katika fasihi,* ) | Anawasilisha utungo wa fasihi simulizi au andishi kwa uketo. | Anawasilisha utungo wa fasihi simulizi au andishi. | Anawasilisha utungo wa fasihi simulizi au andishi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya tungo za fasihi. | Anawasilisha utungo wa fasihi simulizi au andishi kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya tungo za fasihi kwa kusaidiwa. |

| MADA: KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kusoma kwa ufahamu – Vifungu mbalimbali k.v. simulizi, mjadala, shawishi** *(ujumbe na msamiati)* | Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kutambua ujumbe na msamiati kwa utendeti. | Anasoma vifungu vya aina mbalimbali na kutambua ujumbe na msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu na kutambua ujumbe na msamiati. | Anasoma baadhi ya vifungu na kutambua ujumbe na msamiati kwa kiasi. |
| **Kuweza kusoma kwa kina.** *(Novela: maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika, mbinu za lugha)* | Anasoma tamthilia na kutambua maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha kwa utendeti. | Anasoma tamthilia na kutambua maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha | Anasoma tamthilia na kutambua baadhi ya yafuatayo; maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha | Anasoma tamthilia na kutambua baadhi ya yafuatayo; maudhui, dhamira, mandhari, ploti, wahusika na mbinu za lugha kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kusoma kwa ufasaha.** (*matamshi bora, kiwango kifaacho cha sauti, kasi ifaayo, ishara zifaazo*) | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha na kina. | Anasoma kwa kuzingatia vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha. | Anasoma kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vya kusoma kwa ufasaha kwa kuelekezwa. |

| MADA: KUSOMA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kusoma kwa mapana.** *(kutambua na kuchagua matini ya kusoma*, *kutambua ujumbe, msamiati na matumizi ya lugha)* | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua ujumbe na matumizi ya lugha kwa mapana. | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua vipengele vinavyozingatiwa. | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua baadhi ya vipengele vinavyozingatiwa. | Anasoma matini ya kujichagulia na kutambua baadhi ya vipengele vinavyozingatiwa kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini.** | Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini kwa utendeti. | Anatambua vipengele vya ufupisho na kufupisha matini. | Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha matini. | Anatambua baadhi ya vipengele vya ufupisho na kufupisha matini kwa kuongozwa. |

MADA: KUANDIKA

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| **Kuweza kutumia viakifishi mbalimbali** *(herufi kubwa na kikomo, kiulizi, koma, mshazari)* | Anatumia alama ya hisi, herufi kubwa, kikomo, mtajo na mshazari kikamilifu na kwa wepesi. | Anatumia alama ya hisi, ritifaa, mtajo na mshazari kikamilifu. | Anatumia baadhi ya alama za kuakifisha mshazari kikamilifu. | Anatumia baadhi ya alama za kuakifisha mshazari kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha za kubuni.** (vidokezo, *masimulizi, mdokezo, maelekezo, picha, maelezo,)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: lugha, mandhari, wahusika na sifa zifaazo za uandishi, mpangilio wa hatua za insha ya maelekezo, msamiati. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi. | Anaandika aina mbalimbali za insha kwa kuzingatia baadhi ya vipengele vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |
| **Kuweza kuandika aina mbalimbali za insha za kiuamilifu.** (*barua ya kirafiki ya kutoa* | Anaandika aina mbalimbali za insha za kiubunifu kwa kuzingatia vipengele | Anaandika aina mbalimbali za insha za kiubunifu kwa | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya | Anaandika baadhi ya insha za kiubunifu kwa kuzingatia baadhi ya vipengele |

MADA: KUANDIKA

| Viwango / Vigezo | Kuzidisha Matarajio | Kufikia Matarajio | Kukaribia Matarajio | Mbali na Matarajio |
|---|---|---|---|---|
| *mwaliko, hotuba, barua ya kuomba msamaha, hotuba ya kupasha habari, baruapepe)* kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo: muundo, ujumbe, mtindo na kanuni zifaazo za uandishi, sifa za mtu. | vifaavyo vya uandishi kwa utendeti. | kuzingatia vipengele vifaavyo vya uandishi. | vipengele vifaavyo vya uandishi. | vifaavyo vya uandishi kwa kuongozwa. |

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili.** (*Aina mbalimba za maneno;* Nomino za *pekee na za kawaida, Nomino za makundi na za Dhahania, Nomino za wingi na za Vitenzi-jina, Vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi, vitenzi vishirikishi)* | Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa uketo. | Anatambua na kutumia aina mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili. | Anatambua na kutumia baadhi ya aina za maneno katika lugha ya Kiswahili kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi.** (wakati uliopo hali ya kuendelea, uliopita hali ya kuendelea na ujao | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi kwa uketo. | Anatambua na kutumia viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi. | Anatambua na kutumia baadhi ya viambishi vya nyakati na hali katika vitenzi kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua viambishi vya ngeli, ngeli** | Anatambua viambishi vya ngeli, ngeli za | Anatambua viambishi vya ngeli, | Anatambua baadhi ya viambishi vya | Anatambua baadhi ya viambishi vya |

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango** / **Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo.** (A-WA, U-I, KI-VI na LI-YA) | nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo na kwa utendeti. | ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | ngeli, ngeli za nomino na kutumia upatanisho wa kisarufi ipasavyo. | ngeli, ngeli za nomino na kutumia kwa kiasi upatanisho wa kisarufi ipasavyo. |
| **Kuweza kutambua vinyume vya** n**omino na vivumishi kuvitumia katika matini.** | Anatambua vinyume vya nomino na vivumishi na kuvitumia katika matini kwa ubunifu. | Anatambua vinyume vya nomino na vivumishi na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya baadhi ya nomino na vivumishi na kuvitumia katika matini. | Anatambua vinyume vya baadhi ya nomino na vivumishi na kuvitumia katika matini kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali.** *(*kutenda, kutendea na kutendwa*)* | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali kwa wepesi. | Anatambua na kutumia vitenzi katika kauli mbalimbali. | Anatambua na kutumia vitenzi katika baadhi ya kauli. | Anatambua na kutumia vitenzi katika baadhi ya kauli kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia** sentensi sahili na ambatano**.** | Anatambua na kutumia sentensisentensi sahili na ambatano katika matini kwa uketo. | Anatambua na kutumia sentensi sentensi sahili na | Anatambua na kutumia baadhi ya sentensi sahili na | Anatambua na kutumia baadhi ya sentensi sentensi sahili na ambatano |

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Viwango / Vigezo | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| | | ambatano katika matini. | ambatano katika matini. | katika matini kwa kuelekezwa. |
| **Kuweza kutambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha maneno kwa kuzingatia** wakati uliopita, uliopo na ujao | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kuzingatia wakati uliopita, uliopo na ujao ipasavyo na kwa wepesi. | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kuzingatia wakati uliopita, uliopo na ujao ipasavyo. | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kiasi kwa kuzingatia wakati uliopita, uliopo na ujao ipasavyo. | Anatambua maneno yaliyokanushwa, viambishi vya ukanushaji na kukanusha kwa kiasi kwa kuzingatia wakati uliopita, uliopo na ujao kwa kusaidiwa. |
| **Kuweza kutambua na kutumia nomino katika hali ya ukubwa.** | Anatambua na kutumia nomino katika hali ya ukubwa kwa ufasaha. | Anatambua na kutumia nomino katika hali ya ukubwa. | Anatambua na kutumia baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa. | Anatambua na kutumia baadhi ya nomino katika hali ya ukubwa akielekezwa. |

| MADA: SARUFI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Viwango / Vigezo** | **Kuzidisha Matarajio** | **Kufikia Matarajio** | **Kukaribia Matarajio** | **Mbali na Matarajio** |
| **Kuweza kutumia usemi halisi na usemi wa taarifa.** | Anatumia usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu kwa wepesi. | Anatumia usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu | Anatumia kwa kiasi usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kikamilifu. | Anatumia kiasi usemi halisi na usemi wa taarifa katika matini kwa kuongozwa. |

**MWONGOZO WA MIRADI YA SHUGHULI YA HUDUMA YA KIJAMII INAYOCHANGIA UJIFUNZAJI KATIKA GREDI YA SABA**

**Utangulizi**

Shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji (CSL) ni mkakati wa kujifunza kwa vitendo ambao unaunganisha ujifunzaji darasani na huduma kwa jamii ili kuwezesha wanafunzi kufikiri, kupata uzoefu, na kujifunza kutoka kwa jamii. Shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji ni mmojawapo wa mada katika Somo la Kijamii. Mwalimu wa Somo la Kijamii atatarajiwa kuratibu walimu kutoka masomo mengine ili kutekeleza shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji ya darasani. Wanafunzi watatarajiwa kutumia maarifa, ujuzi, mitazamo, na maadili kutoka masomo mengine ili kutekeleza shughuli ya huduma ya kijamii iliyounganishwa. Wanafunzi watashiriki katika mradi mmoja wa pamoja wa darasa wa CSL wakifuata hatua sita kama ifuatavyo:

| **Hatua** | **Maelezo** |
|---|---|
| **Hatua ya 1** | **Utambulizi wa Tatizo**<br>Wanafunzi wanachunguza jamii yao ili kuelewa changamoto zinazokabiliwa na athari zake kwa wanajamii. |
| **Hatua 2** | **Kubuni Suluhisho**<br>Wanafunzi huaandaa njia ya kushughulikia changamoto iliyotambuliwa. |
| **Hatua 3** | **Mpango wa Mradi**<br>Wanafunzi wanagawana majukumu, kutengeneza orodha ya shughuli zitakazofanywa, kuandaa rasilimali zinazohitajika kwa ajili ya kutekeleza mradi, na kuweka ratiba za utekelezaji. |

| | |
|---|---|
| **Hatua 4** | **Utekelezaji**<br>Wanafunzi wanatekeleza mradi na kuweka idhibati wa kazi iliyofanywa. |
| **Hatua 5** | **Kuonyesha Mradi na Kuandika Ripoti**<br>Maonyesho ni pamoja na kuonyesha vitu vya mradi wa wanafunzi kwa jamii na kutafakari kuhusu maoni wanayopokea.<br>Wanafunzi wanandika ripoti inayoelezea shughuli za mradi wao na mafunzo waliyopata kutokana na maoni waliyopewa. |
| **Hatua 6** | **Tafakuri**<br>Wanafunzi wanapitia kazi yote ya mradi kujifunza kutokana na changamoto walizokubana nazo. Wanahusisha kazi ya mradi na dhana za masomo, wakiangazia jinsi dhana hizo ziliwasaidia kutekeleza mradi pamoja na jinsi mradi ulivyosaidia kuimarisha uelewa wao wa dhana za masomo. |

**TANBIHI**: Hatua hizi zitapangwa kwa muda katika mihula mitatu ya kalenda ya masomo.

**Tathmini ya miradi ya shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji (CSL)**
Tathmini kwa ajili ya mradi wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji uliounganishwa utafanywa kwa njia ya tathmini ya mara kwa mara. Tathmini itazingatia mchakato na matokeo ya mwisho. Hii inajumuisha kutathmini kila hatua ya maendeleo ya mradi wa darasa wa shughuli ya huduma ya kijamii inayochangia ujifunzaji. Itatazama vipengele vitatu, yaani: ujuzi kutoka masomo mbalimbali uliotumika katika kutekeleza mradi, umilisi wa kimsingi uliokuzwa, na maadili yaliyokuzwa.

**MUHTASARI WA MBINU ZA KUTATHMINI, NYENZO ZA KUFUNDISHIA NA MAPENDEKEZO YA SHUGHULI NYINGINE ZILIZORATIBIWA ZA UJIFUNZAJI**

| Mada | Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| **Kusikiliza na Kuzungumza** | a) Kumakinikia jinsi mwanafunzi anavyotumia lugha katika mawasiliano<br>b) Kujibu maswali<br>c) Maigizo<br>d) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>e) Kuambatanisha maneno na majibu<br>f) Mijadala<br>g) Mazungumzo<br>h) Matumizi ya ishara za mwili k.v. ishara za uso, za mikono na mabega kuimarisha masimulizi yake<br>i) Wanafunzi kufanyiana tathmini | • Chati<br>• Michoro na picha<br>• Mgeni mwalikwa<br>• Vifaa vya kidijitali (k.v. tarakilishi/vipakatalishi, kinasasauti, rununu, projekta, video)<br>• Mti maneno<br>• Kapu maneno<br>• Vitabu mbalimbali | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Kusoma** | a) Kutunga sentensi k.m. kwa kutumia msamiati lengwa | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni |

| Mada | Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| | b) Kujibu maswali k.m. katika ufahamu<br>c) Kutoa muhtasari wa ufahamu au matini yaliyosomwa<br>d) Kusoma kwa sauti<br>e) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>f) Potfolio<br>g) Shajara | • Rununu<br>• Projekta<br>• Kamusi mbalimbali | 3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |
| **Kuandika** | a) Kuandika tungo mbalimbali<br>b) Wanafunzi kufanyiana tathmini<br>c) Potfolio<br>d) Shajara<br>e) Mijadala kuhusu vidokezo vya insha | • Kielelezo cha insha ya masimulizi<br>• Kielelezo cha insha ya maelezo<br>• Kielelezo cha insha ya maelekezo<br>• Nakala ya barua ya kirafiki<br>• Nakala ya barua rasmi<br>• Barua pepe | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Mijadala inayohusu masuala mtambuko mbalimbali<br>4. Ziara za nyanjani<br>5. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |

| Mada | Mapendekezo ya Mbinu za Kutathmini | Mapendekezo ya Nyenzo za Kufundishia | Mapendekezo ya Shughuli Nyingine Zilizoratibiwa za Ujifunzaji |
|---|---|---|---|
| **Sarufi** | a) Kutambua k.m. kwenye orodha<br>b) Kuambatanisha maneno lengwa<br>c) Kujaza mapengo<br>d) Kutunga sentensi<br>e) Kazi mradi | • Tarakilishi/vipakatalishi<br>• Kinasasauti<br>• Rununu<br>• projekta<br>• Kapu maneno<br>• Mti maneno<br>• Kadi maneno<br>• Picha za vitu mbalimbali<br>• Michoro<br>• Chati<br>• Mabango<br>• Sanamu<br>• Nyenzo halisi | 1. Kazi ya kikundi<br>2. Vyama vya ushirika shuleni<br>3. Ziara za nyanjani<br>4. Kutagusana na vyombo vya habari na vifaa vingine vya kidijitali |